



CHAKULA CHA AKILI

Chenye kuleta mapinduzi ya kifikra.

JITAMBUE WEWE NA KUTAMBUA UKWELI UNAOKUHUUSU WEWE AMBAO HAKUNA
“SUPERIOR” ANAETAKA WEWE UJUE.

N:B Mafundisho haya yameegemea katika nyanja kuu tatu ambazo ni Saikolojia, falsafa (filosofia) na sayansi ya jamii. Lugha kuu iliyotumika ni Kiswahili.

HIZZA ATHUMAN | +255759311893

YALIYOMO.....

(Jumla ya masomo yaliyo ndani ya chapisho hili).

- 1. WEWE NI NANI? NA KWANINI UKO HIVYO ULIVYO.....**
- 2. NINI MAANA YA NENO MAISHA.....**
- 3. KUPUMBAZWA KWAKO WEWE MWANADARASA.....**
- 4. KUJIAMINI.....**
- 5. MAPINDUZI YA MISINGI NA MIFUMO.....**
- 6. MAHAKAMA NDANI YA NAFSI YAKO.....**
- 7. LAWAMA, HUKUMU NA MAJUTO USIYOSTAHILI.....**
- 8. FANYA MAAMUZI SAHIHI NA SIYO YAKUPENDEZA.....**
- 9. NJIA ZA KUSAFISHA UBONGO.....**

CHAKULA CHA AKILI (Mental food)

CHENYE KULETA MAPINDUZI YA KIFIKRA.

Mwalimu wetu katika chapisho hili ataenda kutufundisha kuhusu vitu mbalimbali vinavyohusu maisha ya **BINADAMU** (*human life*), akiongelea maisha ya waafrika kwa ujumla huku akienda mbali zaidi juu ya maisha ya watu wa taifa lake **Tanzania**. Tunaishi chini ya jua hili huku tukiwa kama wasindikizaji, muda umefika sasa twende tukazioneshe akili zetu nyuma ya pazia kuna nini. Hii ni elimu tofauti pengine na zote ulizokwisha kutana nazo katika kuishi kwako na mwalimu ana uhakika wa asilimia zaidi ya mia kuwa hii ikawa ndio Elimu bora katika maisha yako wewe kuweza kukutana nayo.

Kutakuwa na mfululizo wa machapisho haya katika **series** hivyo pale utakapoona kuna umuhimu wa kuzisoma nakala zinazofuatia basi utaweza kuwasiliana na mwalimu kwa kupitia mawasiliano yake. Masomo yanalenga kusaidia kizazi kilichopo ambacho kina macho lakini **hakioni** na pia siyo kwa manufaa ya kizazi kilichopo tu bali kwa manufaa ya kile **kijacho**.

Mwalimu anatumkumbusha kuwa darasa letu halifungamani na upande wowote wa **kisiasa**, *halihukumu*, *halilaumu* bali linatoa **ufumbuzi** (*solution*), Elimu hii haina umri maalumu ni kwa yeyote anaeweza kusoma na kuelewa na kuzingatia pia. Kabla ya kumalizia utangulizi mwalimu anaugusia mshangao wake kwamba;

Maisha ni somo tosha lakini halipo kwenye mtaala (*curriculum*) wowote lakini si vibaya kwa kuona kuna vipande vya somo la hili vipo katika mitaala yote, Wasomi wote na watu wenye IQ kubwa wameshindwa kutupa formula ya maisha, naam! Hakuna formula ya maisha. Lakini kwanini hili Somo watu wanafeli sana lakini pia kwanini tutofautiane kufeli baina ya nchi na nchi au familia na familia wakati wote Somo hili halipo kwenye mtaala kuna nini nyuma ya pazia??.

Twende tukamsikilize mwalimu.

LESSON ONE.

WEWE NI NANI NA KWANINI UKO HIVYO ULIVYO?

Somo hili linahitaji utulivu wa mawazo ili uweze kulielewa, katika somo hili linaanza kwa kutuuliza mimi au wewe kuwa sisi ni nani, majibu ni marahisi sana unaweza jibu mimi Ni mtanzania, au mimi ni mwaafrika au vyovyote utakavoona sawa; **LAKINI** mwalimu wetu anasema ukiulizwa hivo jibu hivi, “*mimi ni kiumbe Hai kinachoitwa Binadamu*”, utajiuliza kuwa kwanini nitangulie kujiita kiumbe hai, Jibu ni kwasababu “**unaishi**” ambapo ndani ya huo mzizi wa neno tunapata neno **MAISHA**.

Unabaki unawaza kuwa kwanini nisiseme tu mimi ni binadamu? mwalimu anajibu kuwa kwasababu neno **HAI** linatupa mwanga wa neno ishi hivyo ukisema mimi ni binadamu tu unaweza kuwa wewe ni binadamu ambae **UPO** Lakini Hauishi, tutaangalia tofauti ya **KUWEPO** na **KUISHI** (*Existing and Living*). Hivyo basi kwa kuwa wewe ni binadamu kama kiumbe hai upo kwenye kundi ambalo kibaiolojia linaitwa **KINGDOM-ANIMALIA--->MAMMALIA**, lakini hauko peke yako kuna wanyama wengine pia ambao mna sifa sawa.

Sasa ni nini tofauti yako wewe na hao wanyama wengine? hapa utawaza utofauti wa kila aina anaoujua **LAKINI** Mwalimu anatuambia utofauti mkubwa uliopo ni kitu kimoja kinachoitwa **REASONING** “*Nafsi inayoishi ndani yako inayokuwa nyuma ya kitendo au tukio lolote ambalo kabla ya kufanyika nje ya mwili wako nafsi inakuletea swali la KWANINI?*” baada ya nafsi hii kuuliza kwanini, basi akili yako itatoa sababu hivyo hupatikana neno lingine linaloitwa **KWASABABU**, hivyo kuishi kwetu kupo ndani ya haya maneno mawili, kwahiyo kila jambo ulilonalo au unalolifanya ni matokeo ya Reasoning.

Kumbe basi huu utofauti wa kuishi tulionao huanza kwa kutofautiana **REASONING**, hii process ya Reasoning huwa inaupa kazi ubongo utumie akili kujibu, kiwango cha akili

kinachokubaliana na ubongo kufanya hii process kinatofautiana kati ya mtu na mtu, hahaha mwalimu *anacheka* kidogo kuona watu wanatumia kiwango kidogo chini ya 20% huku kiwango kikubwa cha ubongo kinachoifanya akili itumike huku kile kinachobaki kinafukiwa kwenye udongo.

Mwalimu anakupa homework ambayo ni kujiuliza kuwa ni asilimia ngapi unazotumia kukamilisha kitendo (process) ya Reasoning?

KWANINI UKO HIVYO ULIVYO?.

Majibu hapa ni marahisi sana ambayo unaweza kuyajibu nayo ni niko hivi kwasababu Mungu kapenda niwe hivi, au niko hivi kwasababu nimependa kuwa hivi au nimejikuta tu niko hivi yote ni majibu **LAKINI** mwalimu anatuambia tujibu hivi niko hivi kwasababu ya misingi niliyoikuta na kuifuata kwa kuiiga, ni misingi gani hiyo na ilianzishwa na nani?, hebu tuangalie kidogo hapa iwapokuwa litakuja kuwa somo kamili katika mfululizo wa masomo haya;

MAPINDUZI YA KIMFUMO (*system revolution*), Koo (Clan) zetu 90% zimetokea katika chimbuko la hali duni lakini siyo zote mpaka leo zina hali duni, kwanini maendeleo yanaonekana kwenye baadhi ya koo? kitendo kilichotokea ni mapinduzi ya kimfumo mapinduzi haya hayafanywi na kundi la wana ukoo bali yanafanywa na mtu mmoja (*a single person*) huyu atafanya **REASONING** process tofauti na wanaukoo wenzake, swali atakalojiuliza linaturudisha kwenye kichwa chetu cha pili katika hii LESSON ONE kinachosema **KWANINI SIS/** tuko hivi na sio vile. Nguvu ya ubongo kusukuma akili nyingi ili isitumie tena 20% kwa ajili ya REASONING inampelekea kufanya maamuzi sahihi ambayo yatapelekea mapinduzi.

Mwalimu anawaangalia ninyi wanadarasa wake anaona sio wao tu wana hali duni pia mpaka wale wanaowazunguka, anaamua kuuliza kuwa nani yuko tayar kuishi nje ya mfumo alioukuta? Majibu ya hapa itakuwa ni homework ya pili.

Mwalimu ngoja akazie kwa mfano huu rahisi kuwa kwa wale waumini wa dini ya kikristo wanaamini kwamba "MUNGU aliuliza kuwa nimtume nani akaokoe wanadamu Yesu

akasema Nitume mimi baba" Leo hii Mungu anakuuliza wewe uyaonae haya kuwa amtume nani kuokoa ukoo /familia yako, kwanini usiseme nitume mimi??. Hivyo basi misingi na mifumo tuliyoikuta inatusababishia hatufanyi **REASONING** itayotoka nje ya mifumo na misingi hiyo.

LESSON TWO

NINI MAANA YA NENO MAISHA

kabla ya kulianza somo hili tujikumbushe kidogo kuhusu ni nini mwalimu alitufundisha kipindi kilichopita, mwalimu alitupa utangulizi wa somo letu (**introduction**), pia mwalimu katika LESSON ONE akatuuliza kuwa sisi ni akina nani, tukapata kutambua kuwa msingi mkubwa unaotufanya tujione sisi ni viumbe hai vinavyoitwa binadamu ni kuwa na uwezo wa kumudu kitendo kinachoitwa (**Reasoning**).

Mwalimu hakuishia hapo katika LESSON ONE bali akatuuliza tena kuwa kwanini tuko hivi? Ndipo alipotupeleka kwenye vitu vinavyoitwa mifumo ya maisha (**systems of life**), na mapinduzi ya kinfumo (**system revolution**). kama haukuelewa kitu usisite kurudia kusoma tena upya, katika usomaji wako tumia Reasoning ili kuipata maana hasa kusudiwa ya Elimu hii.

Baada ya kujikumbusha hayo mwalimu anatutaka tulianze hili somo letu, Somo hili lenye kichwa kinachosema **nini maana ya neno maisha?**. Hapa unaweza kujibu tu kuwa maisha ni kitendo cha kuwepo hai hapa duniani kabla mtu hajafukiwa na udongo, uko sahihi na *MWALIMU* anafurahi kuona hauko mbali sana na maana halisi ya maisha, Mwalimu anakutaka wewe mwanadarasa uwe makini kusikiliza maana ya neno maisha na maneno yanayolizunguka neno maisha ambayo yanaonekana kuwa sawa **LAKINI** si sawa, kuna utofauti ndani yake, ni maneno yapi hayo na utofauti wake ukoje twende tukailishe akili.

Maisha (**life**), tukianza na muhusika mkuu ambao ni neno maisha mwalimu anatuambia **maisha** ni hali inayowatofautisha wanyama (*ambapo hapa binadamu yupo ndani yake*) na mimea kutoka kwenye viumbe visivyo hai (*organic matters*), hali hii ikihusisha kitendo cha kuweza kukua (*growth*), kujizalisha au kuzaliana (*reproduction*), uwezo wa kufanya kazi au vitendo mbalimbali (*functional activity*) na kuweza kupata mabadiliko ndani au nje ya mwili kukielekea kifo (*continual change preceding death*). Mwalimu anatuambia kuwa pamoja na kuwepo kwa maana nyingi lakini hii ni sahihi zaidi.

LAKINI mwalimu kwa kujua ninyi wanadarasa ni wavivu wa kutaka kuishika na kuijua maana ya maisha yenye maelezo mengi anaamua kuwarahisishia kuwa mtu akikuuliza nini maana ya maisha **mwambie** ni hali ya uwepo wa binadamu au mnyama

(*existence of an individual human being or animal*) hawa ndo wahusika wakuu katika somo letu hivyo weka mbali kidogo mimea. Baada ya kupata tafsiri ya neno maisha twende tukaangalie maneno yanayolizunguka neno maisha pamoja na utofauti wake.

Tukianza na maneno haya [KUWEPO](#) na [KUISHI](#) (**Existing and Living**) yana maana au uhusiano gani, mwalimu anasema **Existing** (kuwepo) ni pale mlengwa wetu (mnyama-binadamu) ambapo anakumbana na vitendo mahususi au muhimu vinavyofanywa au kufanyika ili kumwezesha kuwa hai au mzima (*doing necessary to stay alive*).

Vitendo hivyo mahususi au muhimu ni kama kula (**Eating**), kupumua (**breathing**), kulala (**sleeping**), usafi au usalama wa afya (**hygiene**). Hapa sasa wengi wa wanadarasa ndipo walipo kuhakikisha wanaendelea kuliona jua, Reasoning inafanyika ili aweze kuwa hai tu au kuwa mzima, ubongo utasukuma akili yake ilete maarifa ya kuweza kula, na kuweza kuwa na pakulala.

Mwalimu anakuangalia wewe mwanadarasa anaamua kukushangaza kidogo, unajua ubongo wako unasukuma akili ya asilimia 2.6% katika kuwaza kula, asilimia 3.4% kuwaza kuwa na pakulala na asilimia 15% zikikamilishwa na vitendo vingine vinavyokamilisha *Existing*, asilimia 80% badala ya kuzipeleka zinakotakiwa ziende, zinaendelea kupunga upepo kichwani.

Mwalimu anaona kweli vichwa vya wanadarasa wengine ni sehemu tu ya kuhifadhi ubongo, mwalimu anatoa mfano kidogo mtu akisema piga push-up 10, ukifika ya 8 mpaka ya 9 utakuwa umechoka, vivyo hivyo akisema piga push-up 20 ukifika ya 18-19 mikono itakuwa inatetemeka [KWANINI?](#) Kuna kitu kinaitwa "**set of mind**", tutakuja kuliangalia somo lenye kichwa kinachosema **set of mind** katika mfululizo wa machapisho ya Elimu hii.

[ISHI](#) Living hapa ndipo watoto wa kisasa wanaita kujiongeza, ambapo inamaanisha kwamba ni **ubora** (*savour*) wa kila dakika unayokuwepo (**exist**), "*to savour every moment of your existence*" vitendo vinavyofanyika hapa ni kuweza kuona (*taking in the sights*), kuweza kunusa (*taking in the smells*) na kuyaweza mazingira yanayokuzunguka (*taking in the environment around you*).

Ngoja mwalimu akuelezee kwa kina zaidi hapa kuwa kwanza ni lazima ujue kuwa *living* ipo ndani ya *existing* ila ni kujiongeza au kujiboresha zaidi kutoka kuishia

kwenye *existing* tu kisha kufika kwenye hatua nyingine ambayo ni *living* hivyo wanadarasa 100% lakini siyo wote walio kwenye living, huku kujiongeza au kujiboresha (*savour= quality by taste or/and smell*) tunakoongelea hapa kwa kila dakika unayokuwepo (*exist*) unatokana na uwezo unaofanywa na ubongo wako kwa akili yako, huo uwezo uliofichika ndani ya vitendo vinavyofanywa na milango ya fahamu.

Tunaposema uwezo wa kuona (*Taking in the sights*) kuweza kuona vitu ambavyo haviwezi kuonwa na mtu mwingine kwa hiyo si kwa macho haya ya nje bali kwa macho ya ubongo. Hivyo kwa kuwa kila binadamu ameumbwa tofauti ina maana kwamba kila binadamu anacho cha kwake cha kukiona tofauti na mwingine kwasababu hata ubongo wa mapacha haufanani.

Mwalimu anaamua kuuliza wanadarasa *nani ambae ameshakiona cha kwake?* Na je huyo aliyekiona cha kwake anakifanyia kazi? Au unafanya cha mwenzako?, na kama umekiona na unakifanyia kazi lakini ni je unakifanyia kwa asilimia ngapi?. Home workyako nyingine hii.

Mwalimu anamuona mwanadarasa yule umri umekwenda kidogo anajiona hata akikiona saizi hawezi kukifanyia kazi muda umeenda anasikitika sana **LAKINI** anasahau kuwa ana watoto ana nduguze ambao umri uko mahala pake kukiona hicho kilichoumbwa kwa ajili yao, wasaidie kuwakumbusha waweze kuviona utakuwa ni msaada usiofutika utakaokuwa umewasaidia katika maisha yao usisahau tena na tena kuwa Elimu hii ni kwa manufaa ya kizazi hiki na kijacho.

Mwalimu anacheka kidogo kuona kwamba hiki alichokiona cha kukuambia wewe mwanadarasa haya kitatumika vizazi na vizazi, hata akifukiwa leo chini ya udongo moyo wake una amani kwa kutua mzigo mzito kwa faida ya wewe mwanadarasa na yeyote atakae yasikia haya ni wajibu wako kuwafahamisha wanaokuzunguka waweze kuona vilivyopo ndani ya ubongo wao maana wana macho lakini hawaoni wanasubiri neno la kwamba **ONA**.

Sio hivyo tu pia tunaposema uwezo wa kunusa (*smell*) hapa mwalimu anamaanisha kuweza kunusa harufu ya fursa ambayo iko mbali ambayo mpaka wengine wanakuja kuinusa wewe ulishainusa mile tano kabla yao.

Hapa kwenye kuyaweza mazingira yanayokuzunguka, mwalimu anamaanisha nini, mwalimu anaamini kila mwanadarasa ana mazingira tofauti toka anavyoamka na kuanza kutembea mpaka anapofika darasani, mwalimu anauliza *je mazingira uliyonayo yanakutumia au wewe unayatumia?* Je unaona nini kwenye mazingira ambacho wengine hawakioni au unanusa nini katika mazingira uliyopo ambacho wengine wameshindwa kunusa? **AU WEWE UNATUMIKA KAMA MAZINGIRA YA MWENZAKO?** Hiyo ni homework ya pili kwako wewe mwana darasa katika somo hili.

Mwalimu anaendelea kusema tunapozungumzia ubora kwa njia ya ladha (*taste*), mwalimu anamaanisha ni ile ladha ya maisha unayoipata wewe kama wewe katika maisha yako je unapaswa kuendelea nayo na je ni chachu, chungu au tamu? Jibu unalo wewe mwanadarasa.

Lakini siyo maneno hayo tu yanayolizunguka neno maisha kuna neno lingine linaloitwa hai au uzima (*being alive*) lina tofauti sana na neno ishi (*living*) tunapozungumzia neno hai (alive) ni pale mtu anapokuwa zaidi ya kuishi, mtu ambaye amejifunza jinsi ya kuishi (*those who have actually learned how to truly live*), watu ambao wanafanya zaidi ya kupumua (*those who do more than just breath in and out*) huyu mtu tunamuita yuko alive ana uhai wa akili, amekiona alichokuja nacho duniani na ana kifanyia kazi kwahiyu *alive* inakamilisha kitendo cha living "**uhai** unakamilisha **ishi**".

Mwalimu anasema wale ambao walikiona kitu chao na kukifanyia kazi ndio walio na ufaulu wa angalau katika maisha na kwa macho haya ya nje hicho atakachokiona mtu na kukifanya na kisha kikajulikana ndipo hapo washuhudiaji watakitamka kuwa kile ni kipaji, ufaulu wa asilimia kadhaa wa maisha uko ndani ya hiki kinachoonekana **kipaji**.

Mwalimu anakuuliza kama unawajua watu waliotumia kitu cha pekee walichoumbwa nacho na kama kweli wanamafanikio, wale walioitumia sauti kwa kuiona ni kitu cha pekee na hamna mwingine aliye nayo kama ya kwake na akaitumia sauti yake na kama je imempa mafanikio, yule aliyeona miguu yake si kwa ajili ya kutembelea tu kama wengine watumiavyo yeye akaenda mbali zaidi na kama je amepata mafanikio!!??
Homework ya tatu hiyo katika somo hili.

Mwalimu anasikitika kwa kuona pamoja na yeye kuhangaika na [chemistry](#) yake katika level ya chini mpaka ya juu ya elimu akiupa ubongo ushike kile kilichoonwa na wenzie, mwalimu anakuwa mnyonge kabisa kwa kuona hakuweza kufanikiwa hata robo kuyafaulu maisha yake kupitia hicho. Mwalimu anakutaka upaweke akilini hapa maana tutapaongelea kwa kina katika masomo yajayo yatakayogusa hii mnayoiita [ELIMU](#) huko mtaani kwako mwalimu atatujulisha mengi.

Lakini pia ngoja mwalimu agusie hiki kitu muhimu sana kwa wewe kuweza kukijua, kwanini [SUPERIOR](#) ana jukumu moja na huku wewe mwanadarasa una majukumu matatu katika maisha ni yapi hayo? Tutakuja kuliona kwa kina katika machapisho yajayo lakini angalau lijue hili kuwa [SUPERIOR](#) mfumo alionao tayari ni mfumo unaokiwezesha kila kizazi kinachokuja "*huyu aliyepo ni kwa ajili ya yule ajae*" hivo huyu aliyepo jukumu lake ni kuandaa kwa ajili ya kizazi kingine kwahiyo nguvu yote itaelekezwa kwa ajili ya kizazi kijacho kwasababu yeye alikwisha andaliwa na kizazi kilichopita lakini huyu mwenye jukumu moja ndiye anaetumia zile 80% za ubongo.

Huku upande wa pili mwanadarasa majukumu yake yakiwa matatu, yaani wewe mwanadarasa hapo ulipo jukumu lako la kwanza ni kusaidia kizazi *kilichopita hahaha na (na ole wako usisaidie uachiwe laana)*, jukumu la pili ni kuhakikisha wewe unajimudu au umudu familia yako au kwa lugha nyingine ndo ujiandalie maana haukuandaliwa *hahaha (ole wako ushindwe kujimudu ukimbiwe na mke, uchukiwe na ndugu na uwe kero kwa ajili ya shida zako)*.

Jukumu la mwisho ukiandalie kizazi chako kijacho watoto wako *hahaha (ole wako ushindwe watoto wako waje wauane na kukuombea ufe haraka ili warithi hako kakibanda kako)*. Cha ajabu huyu mwanadarasa ndo anatumia 20% ya ubongo wake.

LESSON THREE.

KUPUMBAZWA KWA MWANADARASA.

Mwalimu anaanza kukufundisha somo hili kwa kusema kuwa hapa duniani kuna jela kuu za aina mbili ya kwanza jela inayoonekana kwa macho ya nje (*visible prison*) na ile isiyoonekana Indivisible (*prison*) hapa tutaenda kuangalia hii isiyoonekana. Kwamba pamoja na kujitambua kwasasa kuwa wewe ni nani na pia kujua kuwa kwanini uko hivyo ulivyo na kuelewa neno maisha sasa kwanini hapo kabla haukuyajua hayo yote? Ni kwasababu upo **JELA** na hii jela ndio ile jela isiyoonekana ni ipi hiyo twende tukaiangalie.

Jela isiyoonekana ni jela ya **akili**, **ufahamu** na **maarifa**, jela hii na ile inayoonekana mtumwa wake ni lazima apate **adhabu** au **kutumikishwa** kwa mwanadarasa ambaye amewahi kwenda jela hizi zinazoonekana atakuwa ni shahidi kuwa jela siyo sehemu ya starehe, vivyo hivyo jela hii isiyoonekana inatoa adhabu **kali** adhabu hii ni **HALI** ya maisha ya wewe mwanadarasa.

Mwalimu **hakulaumu** wewe mwanadarasa kwa kushindwa kujitambua na kutambua kuwa kwanini uko hivyo ulivyo siyo hivyo tu bali pia kushindwa kuelewa dhana ya neno maisha ni nini, Kwasababu siyo wewe tu ambaye ni mtumwa wa hiyo JELA bali **JAMII** nzima, jela hii isiyoonekana imewekwa na yule anaeonekana yuko juu yako wewe mwanajamii anaeitwa (**superior**), yuko juu yako wewe mtanzania na pia yuko juu yako wewe mwafrika, utasaidia kumwambia mwalimu kuwa ni nani.

Jela hii imeifunga **akili**, **ufahamu** na **maarifa** **kwa kuipumbaza** hivyo kukulazimisha mwanadarasa kuishi kwa kumuiga **SUPERIOR**. Mwalimu anakutaka wewe mwanadarasa utulize akili ili uweze kupaelewa hapa ambapo panaenda kutuonesha ni nini kilichopo kati yako wewe na **SUPERIOR** na kama hautaelewa usichoke kurudia kusoma tena na tena.

Maisha ya binadamu ni SAFARI, mwalimu pamoja na wewe mwanadarasa tunasafiri, na katika safari hii tunakutana na mabadiliko ya **hali** hivyo inatulazimu kubadili vitu mbalimbali ili tuweze kwendana na mabadiliko ya **hali**. Kinachotokea hapa ni kwamba **SUPERIOR** anabadilika lakini huku akiwa ameipumbaza akili yako isibadilike sawa na yeye bali isubiri yeye abadilike kwanza ndipo wewe uje uige mabadiliko.

Mwalimu anatoa mfano kuwa zamani kulikuwa na wanasayansi na wagunduzi wa vitu mbalimbali kama *Isaac Newton, Michael Faraday, Albert Einstein*, baada ya hivi viumbe muhimu kabisa kuwahi kutokea katika uso wa dunia wengine waliofwata baadae walikuja kuthibitisha michango ya hawa waliowatangulia na kuweza kuongezea au kukosoa palipobidi hivyo pia waliofwata walikuja kuanzia walipoishia wengine.

Hii inakuja kuonesha kuwa maisha ni hatua na kila hatua inayokuja lazima iendelee kutoka kwenye ile iliyoisha (*final stage is the beginning of the next stage*), hivyo ndivyo wafanyavyo SUPERIOR. Mwalimu anakwambia mwanadarasa kuwa **KOSA** halikuwa kujua SUPERIOR anafanya nini, anaishi vipi na ameishia kwenye nini;

KOSA ni kwamba kama yeye na wewe wote mna ubongo tofauti kwanini kila mmoja asitumie akili, ufahamu na maarifa yake kuweza kujua ni nini kinachofuata? Mpaka mwanadarasa unaamua kuwa **MUIGAJI?** na yeye amekwisha kuiunda mizizi ili ujione wewe bila yeye hauwezi kuishi, na anajua kuwa mwanadarasa hutaki kushughulisha ubongo na unapenda vitu rahisi na hakuna kitu **RAHISI** duniani kama **kuiga**.

Hivyo falsafa ya **kupumbazwa** inatokana na kitu kinachoitwa **kuiga**. Mbali na kuanzia ambapo Afrika inamuiga superior, Tanzania inapomuiga superior, bali pia ndani ya jamii inayokuzunguka mwanadarasa kuna mwanajamii mwenzako ambaye unamuiga, naye anaonekana ni superior na mwanadarasa anatamani kabisa kuwa kama huyo *mwanajamii-superior* hapo ndio kabisa mwanadarasa unapozidi kupumbazwa na SUPERIOR mkubwa asiwe na wasiwasi wowote wa kwamba ipo siku utaamka.

Kupumbazwa huku hutambuliwa na nafsi na huku nafsi ikikutaka utoke katika kifungo hicho lakini wingu zito lililokutanda linaipinga, hapa ndipo kinazaliwa kitu kinachoitwa **KUJIAMINI** na **KUAMINI**, mwalimu anakueleza kuwa binadamu yeyote hukumbwa na majibizano ndani ya nafsi yake majibizano haya hutokea baada ya nafsi kuona kile kilichopo ndani ya ubongo na hivyo kukuambia mwanadarasa KIFANYIE KAZI lakini ghafla inainuka nafsi iliyojaa kutokujiamini na kutokuamini (*inferiority complex*) ambayo inakuwa imetengenezwa na SUPERIOR.

Hiyo inferiority complex inakuwa na majibu yafuatayo;

- I. Mbona sijawahi kuona mtu yeyote akifanya kitu kama hiki?
- II. watu wote dunia hii wasingeweza kukiona na kukifanya hadi niwe wa kwanza mimi?
- III. jamii itanielewa kweli? Na itanichukuliaje?

Na majibu mengine Mengi, **HIVYO** hitimisho litakuja kuwa **NISIJISUMBUE** kisha mwanadarasa huenda kufanya kitu ambacho kinafanywa na wanajamii wengine kwasababu anajitengenezea **ulinzi** kuwa *<hata nikishindwa sitakuwa wa kwanza mimi maana wapo waliotangulia kufanya hivo na wakashindwa>*.

Mwalimu anaenda mbele zaidi kuwa kuna msemo wa kifilosofi unaosema "**THE MEANING OF PEACE MEANS THERE'S NO OPPOSITION**" maana ya amani ni kukosekana kwa kipingamizi/upinzani, hivyo wanadarasa wengi mmejaa *AMANI* nafsini mwenu huku mkikosa furaha ya maisha. Kuna kitu hiki ambacho ni muhimu kabisa kukijua.

Wanadarasa wengi hawataki kusikia kitu kinachoitwa sayansi kwa kuona ni kigumu, na ni kweli ni kigumu na ndio maana hakifwatwi, **SAYANSI** msingi wake mkubwa umejengeka kwenye neno **Majaribio** Hivyo ugunduzi wa chochote unachokiona ulianza kwa jaribio hivyo kile nafsi yako inakwambia kwa kukiona ndani yako mara tu kitakapokuja nje ya mwili kitaanza kufanyika kwa njia ya jaribio hapa ndipo tunapata kitu kimoja kinachoitwa **UJASIRI** (*SELF CONFIDENCE*).

Ukiwa nacho hiki na kukisimamia ndipo utakapoweza kuingia kwenye kundi la *HUYU* mtu anaeitwa **SUPERIOR**. Tumepumbazwa katika nyanja mbalimbali katika uchumi, biashara, kilimo, kisiasa na kielimu. Mwalimu atagusia kidogo kwenye elimu maana ndiyo kitako cha hizo nyanja zingine zinazogusa maisha yetu.

Tukiangalia katika Elimu kuna huyu aliyekuwa mtu mashuhuri alieitwa **WASHINGTON CARVER** anakwambia "*Education is the key to unlock the golden door of freedom*"; Elimu ni ufunguo wa kufungua mlango wa dhahabu uliofunga UHURU. Kuwa huru ina maana ufanye kile unachoona wewe mwanadarasa ni sahihi kwa kutumia Elimu yako na si Elimu itumike kufanya kitu kwa kutumia uhuru wako.

TUTAKUJA KUCHAMBUA ZAIDI KWENYE CHAPISHO LITAKALOHUSU ELIMU ambapo tutaweza kuangalia kitu kinachoitwa elimu unayoifuata na kuitumia wewe

mwanadarasa na kujiona una kiwango fulani cha elimu ni **ELIMU INAYOKUPUMBAZA NA SI KUKUZINDUA**, utanielewa zaidi utakapo jifunza **UTOFAUTI KATI YA ELIMU YA "KUFHAMU" NA ELIMU YA "KUTUMIKA**. Ukiona kutakuwa na umuhimu utalitafula chapisho hilo pia.

LESSON FOUR.

KUJIAMINI

Twende hapa tukajifunze kitu *muhimu* kabisa kukijua ambacho ni **kujiamini** ama **ujasiri binafsi**. Hili suala linalogusa kila nyanja iwe ni Elimu, biashara, kilimo ama uchumi na nyanja mbalimbali zinazoyahusu maisha yetu, hapa tutaenda kuangalia kwa ujumla (*in general*).

Twende tukalianze somo letu, moja ya sababu kubwa ya watu kuwa hivyo walivyo ni kukosa/kushindwa kujiamini, tungelikuwa bado tupo kwenye kipindi kama cha karne zilizopita lisingeonekana umuhimu sana, lakini kwa karne tuliyopo sasa iliyojaa **USHINDANI** ni muhimu sana tena sana kulifahamu hili.

Tunapozungumzia **kujiamini** tunamaanisha nini, tumaanisha hivi **uthaminishaji chanya juu yako mwenyewe katika kuweza kufanya jambo fulani** (*your positive self-assessment in performing a task*). Kwa lugha rahisi ni kuamini katika **uwezo** wako binafsi (to believe in your own abilities).

Sote tunajua kuwa vitu vyote vipya vinagunduliwa na binadamu na si paka wala mjiusi bali binadamu, na huo ugunduzi huanza na binadamu mmoja (*a single person*). Kabla ya kutekeleza ugunduzi huo huyu mgunduzi aliwaza kwanza siku zotekitu chochote **huanzia ndani** (kama wazo) **ndipo huja kujidhihirisha kwa nje** (kama kitendo) tutalionza zaidi hili pale katika masomo yajayo.

Baada ya kupata wazo kilichofwata kwa mtu huyo ni kujiuliza je *nitaweza/staweza kufanya? Na nitafanikisha?* Hapa hakuwa na jibu la moja kwa moja bali alijiambia kuwa nitapata jibu baada ya kufanya, kitendo cha kuchukua hatua ya kufanya *hujificha chini ya neno* **kujiamini**.

Kuchukua hatua ya kufanya ndiko tunakoita kujiamini, unaamini katika uwezo wako kwamba **unaweza** kufanya bila kujalisha matokeo yatakuwaje, uwe makini hapa, hamna njia yoyote ya kujua/kuhakikisha kama unaweza au hauwezi jambo fulani pasipo

KUFANYA. Kuna msemo wa kawaida kabisa wenzetu wanasema “*when you start the journey of your professional life, have confidence in your abilities. Because you have not proven your abilities yet.*” < unapoianza safari ya utashi katika maisha yako, jiamini au kuwa jasiri katika maamuzi hayo kwasababu haujahakikisha (*not proven*) uwezo wako bado kama unaweza au laa!.

Mwalimu anakwambia tuliza akili uweze kupaelewa hapa, moja ya kosa kubwa ambalo wanadarasa wanalifanya ni kushindwa kutofautisha au kushindwa kufuata hatua za msingi kuanzia ndani (kwenye kufikiri) mpaka nje (kwenye vitendo). Kushindwa ama kukosa kujiamini kunakuja baada ya kukosa mpangilio kuanzia kifikra mpaka nje (vitendo). Twende tukaangalie tunapokosea;

Unapowaza kufanya jambo lolote hata liwe kubwa kiasi gani, hakikisha hauvuki hatua ya kwanza ni hatua gani hiyo hii hapa, hatua ya kwanza inakuwa kati ya **mawazo** (*idea*) na **kutenda**, mawazo hubeba maarifa (*knowledge*) juu ya hicho unachowaza kukifanya, huwezi kuwaza kufanya kitu chochote bila kuwa na maarifa (*haijalishi maarifa ya kutosha au laah*) juu ya kitu hicho.

Mwalimu alikwisha kuambia kwamba kila kitu kipya tunachokiona huanza kama **jaribio** lakini nyuma ya jaribio kuna kitu kinaitwa **nadharia** (*hypothesis*), hivyo katika hatua ya kwanza ambapo ni **mawazo** na **kutenda** humaanisha **nadharia na jaribio** (*hypothesis and experiment*). Hivyo hupaswi kuvuka hapo kwenye mawazo na vitendo. Hupaswi kuvuka kwenda wapi? Twende tukaangalie hatua ya pili;

Hatua ya pili, **uchunguzi na matokeo** (*observation and results*) baada ya kuwaza na kufanya (*to take an action*) kinachofwata ni uchunguzi wa nini kinachoendelea katika kitendo hicho, Je kinachoendelea kinakupa mwanga wa kuyafikia matokeo uliyoyawaza? Na bila kujalisha ulichokutana nacho wakati wa uchunguzi ulipokuwa unafanya jambo hilo je mwisho umepata **matokeo** gani?.

Kuvuka ama kuruka hatua kunakuwaje ambako ndiko mwalimu anakwambia ni kosa kubwa na kunapelekea ushindwe kujiamini na kisha unashindwa kufanya kabisa jambo hilo ni hivi;

Mwanadarasa anapokuwa katika hatua ya kwanza ya mawazo huruka hatua zingine zote zinazofwata na kwenda moja kwa moja kwenye hatua ya matokeo, yaani yeye hujipa hatua mbili tu (mawazo na matokeo) “hahaha, *hatari sana! Wala Mwanadarasa hataki kusumbua akili yake anajirahisishia na kujipa hatua mbili tu anaamua kupita short cut*”

kinachofanyika hapo ni Mwanadarasa kujipa matokeo mwenyewe kwenye kichwa chake bila kitendo kufanyika, ana heri yule anaejipa matokeo chanya kabla ya kitendo maana huyo ndiye aliyejaa kujiamini (*Over confidence*) lakini huyu tunaemzungumzia hapa yeye matokeo ambayo hujipa ni **hasi**. Hivyo hushindwa kabisa kukifanya hicho kitu kwasababu ya kujipa matokeo mwenyewe.

Anauona uwezo wake hauwezi kufanya jambo hilo pasipo hata kuujaribu, matokeo yake jamii inakosa ugunduzi wa vitu mbalimbali, jamii inakosa uanzishwaji wa vitu vipya tunarudi kulekule tunaishia **kuiga tu**. Hivyo mwalimu wako anakwambia wewe mwanadarasa **HAUNA UHAKIKA JUU YA UWEZO WAKO KWAMBA UNaweza AU LAAH NI MPAKA UMEFANYA.**

Kiuhalisia ni ngumu kuanza kuyatekeleza mawazo yako kwa kuanza na 100% za kujiamini (*confidence*), kujiamini huimarishwa na kuanza kuchukua hatua ya kufanya. Unaweza ukawa shuhuda hapa ukamsikia mtu anasema *nilikuwa nakihofia tu bure kukifanya hiki kumbe kirahisi tu*.

Kuna mwanafilosofia mmoja anaitwa Plato anasema “*The beginning is the most important part of the work*” kumbe kitu cha kwanza kabisa katika kufanya jambo lolote ni **KUANZA** (*beginning*). Au kwa lugha nyingine tunaweza kusema **uthubutu** na ni hatua moja muhimu sana ya kujenga kujiamini (self-confidence). Aina ya pili ya kutokujiamini ambayo pia ina wanadarasa wengi ambao wengi wameiweza ile ya **uthubutu** wa kuanza kufanya jambo ni hii hapa twende tukaiangalie;

Aina hii ya pili huja baada ya mtu kuanza kufanya, anapoianza hatua ya pili ya uchunguzi juu ya mwelekeo wa kile alichokikusudia, uchunguzi wake ukibeba hasi nyingi basi kujiamini kote kunatoweka, anaishia hapo na hiyo hujijenga na kuwa **TABIA**, huyu jamaa Michael Jordan anasema;

“if you quit once it becomes a habit. Never quit” ndio maana utamsikia mtu anasema *nimejaribu kufanya vitu vingi kwenye haya maisha* lakini ukimwalia hana hata kimoja mkononi. Watu wanashindwa kusimamia kile wanachokiamini. Watu wanashindwa kuwa wavumilivu [Jean Jaques](#) anasema *“patience is bitter but its fruits is sweet”*. Mtu anatamani aanze kufanya jambo leo kesho aone mafanikio.

Mwalimu anakwambia safari ya mafanikio katika maisha ni kama *kilimo cha miti tena ya mbao* huwezi kupanda na ukatarajia kuvuna ndani ya miezi miwili au mitatu ijayo. Lakini kuna sababu kadhaa zinazopelekea watu kushindwa kujiamini au kupoteza kujiamini, tutaenda kuziambia chache ambazo ni muhimu sana.

Tukianza na ya **kwanza misingi uliyojengwa nayo mwanadarasa**, watu wengi wamejengwa kwenye msingi **kawaida** ama mazoea (*utakuja kupata maelezo ya kina juu ya misingi katika masomo yanayofuata*), mwanadarasa haamini kama anaweza kufanya jambo ambalo halijazoeleka katika jamii, na kwa kuwa mwanajamii yeyote amejengwa katika msingi wa kutokuwa na **uthubutu** hivyo huyu mwanadarasa haamini kama anaweza kuthubutu na kufanya kitu tofauti na wengi walivyozoea.

Wanadarasa walio wengi wanaishi maisha ya kuwapendeza watu (*to please people*), kabla ya kufanya chochote mwanadarasa anakuwa na maswali ya kijinga kabisa kichwani, mwalimu lazima awe mkali kidogo hapa, maswali yenyewe ni kama haya *moja* wengine watasemaje (*what will others say?*) Mbili je Watu watanicheka (*will people laugh at me?*) Tatu nitawatazamaje watu endapo hili jambo litafeli (*how can I face others if fail?*) Na maswali mengine mengi mwalimu anayaita ya **kijinga**.

Kuna msemu mujarabu kabisa unasema *“Don't be afraid to stand for what you believe in, even if that means standing alone”* <usiogope kukisimamia kile unachokiamini hatakama unaona umesimama peke yako hamna anaejali> hivyo ndivyo mwanadarasa inatakiwa uwe na mwalimu anakwambia **toka** kabisa kwenye msingi **kawaida** unaokuongoza ujiwaze katika kufeli.

kuna huyu jamaa anaitwa [Bill Cosby](#) anasema *“In order to succeed, your desire for success should be greater than your fear of failure”* <ili kuweza kufanikiwa, matamania ya kufanikiwa yanapaswa yawe makubwa zaidi kushinda hofu ya kushindwa>. Kwanini mwalimu anazungumzia zaidi wanadarasa kushindwa kujiamini katika kufanya mambo

mageni/mapya, kwasababu wengi wa wanadarasa hawapati taabu sana kujiamini kufanya mambo yaliyozoeleka katika jamii.

Na Kwanini watu hujiamini kufanya mambo ambayo tayari yamezoeleka kwasababu wanajiona kupata ulinzi wa jamii kwamba kwa sehemu yoyote mwanadarasa atakayokwama basi hatakoswa wa **KUMUULIZA**, lakini kwenye kufanya jambo jipya anajiona ataonekana kichaa mbele ya jamii na ni kweli mwanafilosofia mmoja anaeitwa [Aristotle](#) anasema “*no great genius has ever existed without some touch of madness*”. Hivyo usiogope watu watakuonaje ni wajibu wako kuwashangaza watu (*to prove them wrong*).

Sababu ya pili ya watu kushindwa kujiamini, kukosa maarifa na ufahamu wa kutosha juu ya kitu wanachopanga kukifanya, (*lack of enough knowledge and good understanding*). Mwalimu anakwambia kwamba watu wengi hushindwa au hukosa kujiamini kwasababu hawana uelewa wa kutosha juu ya kufanya kitu fulani, kwasababu wapo kwenye msingi wa **kuiga**, basi kila atakachotaka kukifanya hawezi kuwa na uelewa wa kutosha juu ya hicho kitu, wengi wao husita kufanya kabisa lakini wale ambao hulazimisha kufanya basi hufeli vibaya kiasi kwamba wanashindwa kuinuka tena kisha mtaani watu huwapachika majina kuwa **mkurupukaji**.

Hata iwe biashara tutakuja kuangalia vizuri pale mwalimu atakapotoa chapisho linalojikita kuielezea Nyanja ya biashara, kabla ya kuanza biashara yoyote hakikisha unataarifa zote muhimu (*details*) za kuihusu biashara hiyo. Moja ya kitu **wanadarasa** walio wengi wanashindwa kukizingatia na ni kitu muhimu basi ni **kutenga muda mchache** wa kutafuta kukijua (*doing research*) juu ya hicho anachotaka kufanya na kuruhusu hisia za kukuona ukifanya hicho kitu zikikuongoza.

Sababu ya tatu kushindwa kuuishi wakati uliopo, watu wengi miili yao inaishi wakati uliopo huku mawazo na fikra zao zinaishi wakati uliopita (*past*). Wengi wao kipindi fulani kilichopita walijaribu kufanya vitu viwili vitatu na viliwaletea matokeo mabaya sana, ile hali ikawaharibu kisaikolojia na wakakubali kuishi nayo. Bado mwanadarasa anajiona ni yuleyule aliyeshindwa kipindi kile, bila kujalisha sababu zilizofanya ashindwe kipindi kilichopita, bila kujalisha kuwa kwasasa ufahamu umeongezeka kiasi gani.

Mwalimu anakwambia mwanadarasa **uishi usasa achana na ukale**. Maarifa uliyonayo kwasasa ni tofauti na yale yaliyopita, kale haina cha kufanya nawewe, historia haibadilishi chochote juu yako (*past has nothing to do with you*). **Karl marx** anasema;

“it is not history which uses men as a means of archiving-as if it were an individual person- its own ends. History is nothing but activity of men in pursuits of their ends”.

Kataa kabisa kuishi kutokana na historia mwanadarasa ***“Stop being a prisoner of your past. Become the architect of your future”.*** **By Robin.**

LESSON FIVE

MAPINDUZI YA MISINGI NA MIFUMO

Twende tukalianze somo letu hili, umakini na utulivu unahitajika lakini pia **ukweli** ni mchungu jitahidi tu uuelewe ndio sifa ya dawa ilivyo *“The art of medicine consists in amusing the patient while nature cures the disease.”* -By Voltaire.

Katika masomo yaliyopita mwalimu aliweza kugusia msingi **kawaida**, kuwa watu wengi wamejengwa katika huo wakiamini katika kufanya kile tu kilichozoeleka kufanywa katika jamii. Mwalimu alisema wengi wao hufanya hivyo kwasababu ya kujitengenezea **ulinzi** kuwa hata akifeli hataonekana yeye wa kwanza kufeli, au akikwama mahali atakimbilia kuuliza wafanyaji wengine wa hicho kitu na si kutaka akili yake ipambane **yenye** katika kutatua hilo.

Mwalimu anakwambia kutokana na hali hiyo kinatengenezeka kitu kinachoitwa **utumwa wa kifikra** kwamba unaona jambo fulani haliwezekani pasipo **mawazo/fikra** za mtu fulani. Hapa huchagizwa sana na kitu kinachoitwa **kujiamini** (*self confidence*), mwalimu anakuambia kuwa kinachobaki ni kusubiri kwanza **superior** afanye ndipo nasisi wanadarasa tuige.

Leo twende tukaangalie misingi **mingine** ambayo hupaswi mwanadarasa kwenda nayo, msingi wa pili **msingi maumivu** uwe makini hapa, watu wengi wanakosa **tafsiri na maana** sahihi ya vitu wanavyovisikia na kufanyika, matokeo yake watu huteseka huku wakifurahia utofauti wa mateso yao. Utulize akili kwelikweli hapa kuna kazi kubwa mpaka kufikia ngazi ya superior.

Baada ya waafrika ama watanzania kuupata **uhuru** wa bendera kwamba tujitawale wenyewe kuna utumwa tulioachiwa ambao huo kuuona ni ngumu kwasababu tumeweka kuwa msingi wa maisha na kuoneka ndio uhalisia wa namna ya kuyafikia mafanikio. Wanadarasa walio wengi wamekuwa **watumwa** wa shughuli wanazozifanya

kila siku shughuli za kuwaingizia kipato na kuwafikisha kwenye mafanikio. Kuna baadhi ya kauli na misemo iliyozoeleka kabisa katika jamii, mojawapo ikiwa ni **ili uweze kufanikiwa ni lazima uumie (upate maumivu) ama uteseke.**

Huku msembo wa pili ukiwa ni *ili uweze kufanikiwa lazima uvuje jasho haswa “hahaha”* ngoja tu mwalimu acheke kidogo maana kitu kinachoenda kufanyika hapo watu wanaenda kuumiza ama kutesa **mwili** maskini ya Mungu na si kuumiza **akili**. Watu wanaenda kuvuja jasho la mwili mpaka likikauka ngozi inabaki na **chumvi** “hahaha” na si kuvuja jasho la akili. Usichanganye maneno kuna **mazoezi** na **kazi**

Ukiachilia mbali vitu vinavyofanywa katika kazi fulani ambavyo vinahusisha **nguvu** ya mwili, kwa mfano mtu anaweza kuwa mchezaji na vitu vingine ambavyo hata akienda kwa daktari hatashauriwa kufanya mazoezi kwasababu mazoezi ndiyo namna ya ufanyaji kazi wake. Lakini kuna kazi ambazo huyu daktari kabla hajafahamu ufanyaji wako atakuagiza ufanye mazoezi kwasababu hiyo kazi si ya kutumia nguvu, lakini cha ajabu wewe ndio kazi ambayo jasho linakauka na kuacha chumvi tu juu ya ngozi.

Mpaka leo kazi zinazopaswa kufanywa na **mashine** bado zinafanywa na nguvu ya mwili, lakini cha ajabu kabisa hata kazi ambazo zinatakiwa kufanywa na **wanyama** nazo zinafanywa na nguvu ya mwili wa binadamu, kazi anayopaswa kufanya **punda** cha ajabu inafanywa na wewe mwanadarasa “*hatari sana hii*” Mungu wanaemwamini hawa wanadarasa awasaidie kuweza kuielewa hii elimu.

Mwalimu anakupa homework kidogo nenda kafanye utafiti (*research*) kati ya wale wanaotumia nguvu nyingi ya mwili na yule anaetumia nguvu nyingi ya akili katika kutekeleza shughuli yake yupi anamafanikio. Mungu kaumba uwezo mkubwa ndani yako mwanadarasa wa kuweza kuvitawala viumbe vingine tofauti na wewe, lakini cha ajabu hauvitumii hivyo viumbe na vimekuwa kwenye level moja ya maisha na wewe.

Katika ufanyaji wa shughuli mbali mbali akili na nguvu ni lazima vitumike lakini kwa uwiano gani? Mtu atakwambia mwalimu najua ili niweze kulima na kufanikiwa nisitumie tena jembe la mkono, mwalimu najua ili niweze kufanya kwa uharaka na ufanisi inanipasa nitumie msumeno wa mashine wa kuchania mbao na si kuchana kwa msumeno wa mkono, lakini tatizo mwalimu ni kwamba sina uwezo wa kuwa na hizo mashine. Sasa tunafikaje kote huku!

Moja ya kitu ambacho kila mwanadarasa anakijua basi ni suala la **muda**, mwanadarasa anaamini kwamba ili uweze kufanikiwa ni lazima ujali muda, ni kweli lakini huyuhuyu mwanadarasa ukimuuliza ni jinsi gani anavyopoteza muda hawezi kukuelezea.

Kupoteza muda namba moja hapa duniani ni kufanya kitu ambacho unaijua picha ya mwisho wake kuwa hutofikia mafanikio ya kutosha lakini unajipa moyo na **kauli** za kijinga kabisa kwamba **lolote linaweza kutokea mbele ya safari**. Utaanzaje kilimo kwa namna ambayo mwenyewe ukiangalia unaona hata ufanye kwa miaka mitano mfululizo bado hautafanikiwa? Utaanzaje kazi ambayo unaona hata ukiifanya kwa miaka sita bado utakuwa unahangaikia tu tumbo lako? Huku ndo **kupoteza muda**.

Sehemu kubwa ya wanadarasa wengi wanapokosea ni **mwanzo**, mwanzo wa ufanyaji wa kila shughuli wengi wao hawaanzii mwanzo kwanini, kwasababu hawaujui mwanzo na kwanini hawaujui huo mwanzo sababu **kuu** ni hii hapa;

Wanadarasa wengi wamefumbwa hapa, leo mwalimu anaenda kukufungua, wengi wa watu kabla ya kufanya shughuli yoyote ile iwe biashara ama kilimo au kitu chochote, kitu cha kwanza anachoumiza kichwa ni kupata **mtaji**, kosa moja kubwa sana kumbe kitu cha kwanza ambacho ulitakiwa uumize kichwa kuwa utakipataje ni **maarifa** (*knowledge*) inayoihusu kitu hicho. Tofauti yako na **superior** ni kwamba wewe unawaza kwanza upate mtaji ndipo uanze kuuliza kuwa kitu fulani kinafanyikaje ndio maana kundi kubwa la watu hujikuta wanafeli.

Ni kawaida mtu kusikia anaomba msaada wa fedha ili aweze kufungua genge lakini mwalimu na utu uzima huu hajawahi kusikia mtu akiomba msaada aweze kupata fedha ya kumuwezesha kupata **maarifa** ya biashara ya genge, sikiliza vizuri mwanadarasa hakuna kitu kinachofanyika bila ya kuhitaji maarifa juu ya ufanyaji wa hicho kitu hata kama kinaonekana ni kidogo kiasi gani.

Kwanini wanaoupa mtaji kipao mbele na si maarifa ya kutosha kwanza wanafeli ni kwasababu moja ambayo ni hulka ya milango ya fahamu kivipi, ni kwamba mwili wa binadamu umeumbwa na matamania (*desire*) haya matamania huzaa tamaa, mtu akishapata mtaji tamaa yake kubwa nikuona kashaanza kufanya hiyo shughuli, kuna kitu kimoja anachokimbizana nacho ambacho ni hofu (*fear*). Anahisi huo mtaji ataweza utumia

kwa kitu kingine ambacho ni tofauti na hicho anachokipanga hivyo hana budi kuanza kufanya haraka iwezekanavyo.

Sifa ya yule anaeanza na maarifa kwanza hatahitaji mtaji mkubwa kwasababu hata akipata shilingi mia tano anajua sehemu yake husika ya kuipeleka. Na hata akianza na kiasi kidogo sana ana malengo ya kufika kwenye umilionea kwasababu anajua njia anayopita. Kwanini watu ni ngumu kuanza na kutafuta maarifa kwanza, sababu ya kwanza ni kushindwa **kujiamini**. Wanaofanikiwa siku zote huanzia kwenye **hamna** kwenda kwenye **kuwanacho** (*from nothing to something*). Picha iliyojengeka kwenu ninyi wanadarasa hamuamini katika **nothing**. Hivyo kutafuta maarifa kwa kitu ambacho haujui hata mtaji utatoka wapi ni kumletea masihara huyu mwanadarasa.

Kwasababu hiyo utamkuta mwanadarasa anakifanya kitu kwa njia ile ile zaidi ya miaka 10. Inakuwaje unajisifu mbele za watu kabisa kuwa mimi nimekuwa muunga pancha za baiskeli kwa mwaka wa nne huu sasa. Hivyo kwanini hali iko hivyo ilivyo ni kwasababu watu wamejengwa hivyo, hawajajengwa katika mfumo wa maarifa kwanza. asilimia 70% ya wanadarasa wanafanya vitu ambavyo hawana uelewa navyo wa kutosha.

Maarifa mengi yamejaa kwenye nakala mbalimbali lakini kutokana na desturi tuliyojiwekea ya kutoyatafuta, hizo nakala huwa tunazifungia maandazi. Acha **ujinga** wa kutotaka kuuacha **ujinga** jifunze kutoa gharama kwa ajili ya kupata maarifa. Kitu ambacho ulitakiwa **kukiandalia** gharama ya kutosha ni **elimu juu ya** vitu mbalimbali na sio kuweza kugharamikia ili uweze kujua ugomvi wa jirani yako. kuna watu wawili hapa kuna atakaeweka bundle ili apige kujua misha ya jirani yake yanaendaje na huku mwingine akiweka bundle aweze kuingia mtandaoni asome kupata maarifa.

Hivyo tafuta kuwa na mwanzo sahihi wa kitu chochote unachopanga kukifanya na huo mwanzo ni ngumu kuujua isipokuwa umetafuta maarifa ya kutosha kukihusu hicho kitu. Usianze kufanya kitu ili mradi, kijue kwanza ndo ukifanye. Jitoe gharama kwa ajili ya kutafuta maarifa na maarifa yote yanapatikana kwenye maandishi.

Una macho ya kuweza kuona yatumie ipasavyo yasiishie kuona vitu vya kijinga ama kukesha kusoma vitu vya kijinga ambavyo hata mwanao au mjukuu wako akikuuliza nini unasoma utashindwa kumjibu. Soma kitu kitakachokufanya uweze kujua yale ambayo huyajui lakini ukiyajua itakuwa faida kwa watoto wajukuu na vitukuu vyako pia.

Ukianza kitu cha kufanywa na mashine kwa kufanya kwa mkono baada ya miezi kadhaa hakikisha unafanya kwa kile inachostahili kufanywa nacho.

Principal ni moja tu “to know a lot, read a lot”.

LESSON SIX

MAHAKAMA NDANI YA NAFSI YAKO (HUMAN SPIRITUAL INNER COURT).

Mwalimu anaanza kwa kuelezea maana rahisi ya kitu kinachoitwa mahakama, kuwa ni sehemu ambapo tunapata **HUKUMU** ya tatizo lilitokea kwa kufuata haki chini ya sheria fulani iliyowekwa ili kuleta usawa, suluhu na amani katika jamii husika. Tutajikita zaidi kwenye neno hukumu kama ambavyo limeandikwa hapo juu.

Ndani ya mwili wa binadamu kuna kitu ambacho wanafilosofia tunakiita **CONSCIENS** tunasema ni sauti ya ndani kabisa inayomuongoza mtu kwenye kipi sahihi afanye na kipi si sahihi asifanye (*an inner voice or feeling viewed as an acting as guide to the rightness or wrongness of one's behaviour*), hii sauti mara nyingi hupuuza (*ignored*) baada ya matokeo ya kile ulichoenda kukifanya kuwa sivyo ulivyotarajia, hii sauti inakupeleka kwenye mahakama ambayo ni **nafsi** kisha unaanza kuhukumiwa ndani, baada ya tukio lote hilo kufanyika kinakuja kitu kinachoitwa majuto (*regression*).

Kumbuka vitu vyote hivi vinafanyika ndani yako, hapa mwanadarasa utakuwa shahidi pale muda mwingine unatembea uko peke yako lakini unajiona kama uko na mwenzako kama mnapiga soga kabisa mwisho mtu anaweza hata kucheka peke yake, hivyo kipindi hayo yote yanafanyika ni ngumu binadamu mwingine kujua kwasababu kipindi vinafanyika vyote hivyo mwili wa nyama huendelea na majukumu yake kama kawaida.

Majuto haya huja kujionesha kwa hali ya nje ya kimwili ambapo mtu huyo anakuwa na msongo wa mawazo (*stress*) na pia huwa mwenye hasira au mnyonge kitu ambacho kinaleta madhara pia kwa binadamu ya kiafya kama Magonjwa ya moyo na mengineyo.

Mwalimu anatoa mfano kidogo;

Mfano huu nitautoa kwenye mlengo wa **mapenzi**, inawezekana mwanaume ambae yupo **ndani** ya mahusiano lakini akapita sehemu na kumuona mwanamke flani akavutiwa nae kisha akaamua kwenda kumtongoza, hiki kitendo cha kwanza lazima kitaambatana na sauti nyingine nyuma ndani yake inayomwambia

MBONA UNAE LAKINI WA KWAKO ataamua kuipuuza, baada ya kumtongoza huyo binti, akiulizwa swali labda kweli *hauna mwanamke mwingine?*

Mwanaume atakachojibu kuwa **SINA**, lakini kutakuja sauti nyingine ndani yake inamwambia **ACHA UONGO MBONA UNAE** kumbuka huyu mtu anafanya majibizano bila mwanamke kugundua, hivyo huyu mwanaume anaweza kukubaliwa na mwanamke, sasa ikijatokea labda mwanamke ni mwathirika na huyu mwanaume mwisho wa siku amekuja kuambukizwa ugonjwa.

Hapo ndipo maneno yafutayo yanapojitokeaza na maneno hayo huenda nawewe mwanadarasa umewahi kumbana nayo katika tukio lolote flani lilikutokea maneno hayo ni kama;

- i. **Lakini Moyo ulisita sana kufanya**
- ii. **Nilihisi haya yangetokea**
- iii. **Nilijua tu.**

Na maneno mengine mengi, hivyo hufanya kwenye nafsi yako kutawaliwe na migogoro kumbuka siyo tukio moja unalopata matokeo hasi, hivyo moyoni mwako kunakuwa na mlundikano wa **Lawama** na **majuto**. Sauti hii hupuuza katika nyanja nyingi zinazohusu maisha ya binadamu, sauti hii hupuuza pia hata pale binadamu anapofanya shughuli ya kumuingizia kipato. Nini sababu ya sauti hii kupuuza twende tukaiangalie;

Sababu ya sauti hii ya ndani (*inner voice*) kupuuza ni kutokana na msingi wa maisha wewe mwanadarasa uliojengwa kwa huo, msingi ambao unasimamia kwenye neno **kawaida** yaani kila utakachokifanya ni kitu ambacho kimeshafanywa tayari kitu ambacho kinakutaka upitie hatua moja mbili tatu zilizowekwa tayari ili uweze kufika, **HUKU** ukisahau hizo hatua hazikuwepo kabla isipokuwa ni mtu aliziona ndani ya ubongo wake na kuziweka hadharani leo hii inakuwa ndiyo njia (**PATHWAY**) ya wewe kupita.

KAWAIDA tunayozungumzia hapa ni kawaida ambayo jamii nzima imejengwa kwa hiyo, ambapo ndani ya jamii tunakutana na kauli hii "ili uweze kufanya hiki kitu kwa **kawaida tunafanya hivi**" lakini tunasahau huyo mwasisi wa hiyo inayoitwa kawaida ni mtu mmoja. Mfano wa kawaida mojawapo, *mtoto anaefaulu darasa la saba*, akafaulu na *form four* kisha *form six* na kwenda chuo kikuu moja kwa moja huyo ndio mwenye akili"

Lakini huyu ambaye ataenda kukisomea kitu ambacho ndicho amejaaliwa nacho na kukibobea kabisa na kisha kuwa mtaalamu wa hicho basi mtu huyo hataheshimiwa kama msomi, wala hataheshimiwa ama kuonekana ni mwenye akili kwasababu hajapita kwenye hiyo njia ya **chuo kikuu**, ila tu ataonekana anajua kitu fulani, hiyo ndio kawaida ambayo jamii imejengwa kwa hiyo, na kawaida zingine unazozifahamu wewe mwanadarasa.

Sababu nyingine inayofanya sauti hiyo ipuuzwe, ni kuusikiliza mwili wa nje ambao umejengwa ndani ya dhana ya kuamini kile tu ambacho kimekwisha kutokea. Hivyo kuamini kile ambacho hakijatokea bado huwa ni ngumu kwasababu mwili huu huona kama unaenda kinyume na uhalisia. Lakini pia huu mwili wa nje unaoongozwa na milango mitano ya fahamu ambapo hujitokeza neno **tamaa** kwa kuona au kusikia, pia hii nayo ni moja ya sababu inayopelekea kuipuuza hii sauti.

Mpaka hapo tunaweza tukatenganisha haya makundi mawili makubwa, la kwanza;

Kundi la kwanza Sauti hii inapuuza na msingi ambao umemjenga mwanajamii ambao uko juu ya neno **kawaida**, hapa uhusika zaidi na kupuuza sauti inayohusika na shughuli za kuyajenga maisha zinamuingizia mtu kipato.

Kundi la pili sauti hii inapuuza na mwili wa nje unaoongozwa na milango ya fahamu ambapo tunapata neno **TAMAA** hapa panahusika na shughuli zinazohusu hisia kama **mapenzi** (*love affairs*).

Athari ya jumla ni kwamba unaupa ubongo ubize wa kushughulika na kazi ambayo haukupaswa kushughulika nayo, ubongo wako na wa **SUPERIOR** unakuwa uko bize ila tofauti ni aina ya ubize, mbeleni tutaangalia ubize wa superior ni upi wakati wewe mwanadarasa ubize wako ni kusuluhisha hiyo migogoro. Hivyo baada ya Sauti hii kupuuza kinachokuja kufwata ni **LAWAMA** na **HUKUMU** ndani yako ambayo huendeshwa na mahakama ambayo ni **NAFSI** yako.

Lakini Lawama na Hukumu hii huwa inakubaliwa katika kundi la pili kwa maana nyingine kujutia kunakubaliwa katika kundi la shughuli za kihisia **KWANINI** na pia vipi kuhusu kundi la kwanza ambalo linahusika na shughuli za utafutaji je majuto yanakubaliwa?? Na vipi kama niliisikiliza sauti na bado nikapata majibu hasi???

Tutaenda kuanza na kundi la kwanza kwenye sababu za kupuuza sauti ya ndani (*inner voice*) Hapa tuliongelea kwamba mwanadarasa amejengwa katika msingi ambao shughuli zake azifanyazo kila siku ili aweze kuwa hai (*to be alive*) basi shughuli hizo ni zile za **KAWAIDA** ambazo tayari zipo na zinafanywa katika jamii, au kwa lugha rahisi zinafanywa kwa mazoea au zimezoeleka kufanyika katika jamii, hebu tazama kulia na kushoto mwanadarasa hicho unachokifanya kikoje au nawewe unakifanya kwasababu umekuta kipo kinafanyika?.

Basi hapo utakubaliana na mwalimu kuwa unalitukuza neno **KUIGA**, kama mwalimu alivyolizungumzia katika masomo yaliyopita, na kwa njia hiyo unazidi kumpa raha SUPERIOR. Tuangalie Jinsi ya kutoka kwenye huu msingi uliojengeka kwenye neno **KAWAIDA** au mazoea ni kuiruhusu akili yako iende mbali zaidi kufanya **REASONING** nje ya zile 20%, kwasababu kuendelea kudumu katika msingi wa neno **KAWAIDA** au mazoea. **REASONING** inayofanyika hapo ni chini ya 20% kwasababu akili inaenda kwa **KUIGA** ambapo hapo kutajitokeza neno lingine linaloitwa "**ULIZA**"

Neno ULIZA ni kijimsingi kidogo ndani ya msingi **KAWAIDA**, kijimsingi hiki kinaenda kinyume na **REASONING**, wakati kitendo cha reasoning kimesimamia neno **KUJIULIZA** huu msingi unaenda kusimamia kwenye kijimsingi kinachosimamia neno **ULIZA**, haya ni meneno mawili tofauti ambayo moja linakutaka wewe utumie uwezo wako huku lingine likikutaka utumie uwezo wa mwingine, na nirahisi kutumia uwezo wa mwingine kwasababu kitu ni **KAWAIDA** kimezoeleka hapa ndipo mwanadarasa anapokuwa na **utegemezi wa kifikra na utumwa wa kifikra**.

Mwalimu anakukumbusha mwanadarasa kuwa mtu tunaemzungumzia hapa ni yule ambae anataka kufaulu maisha kwa njia halali (*legal ways*), hivyo mwalimu hahusiki na wale ambao kuyamudu maisha ni kwa njia ambazo ziko nje ya **UBINADAMU**.

Kutokana na kuwepo ndani ya msingi **KAWAIDA** mwanadarasa lazima ufeli maisha, wote unaowaona ambao wako ndani ya msingi huu hawapo hata kwenye 10% ya kufaulu maisha yao mwanadarasa anaweza kuona kuwa mbona wapo ambao wapo kwenye huu msingi ambao wanajishughulisha na ualimu kwasababu walikuta kuna kitu kinachoitwa ualimu au ni polisi kwasababu walikuta kitu kinachoitwa polisi na wana nyumba na usafiri wa kutembelea mwanadarasa ukaona hawa watu wamefaulu;

Mwalimu anakwambia mwanadarasa kuwa hawajafaulu hivyo kipimo cha kufaulu maisha ni nini??

Twende tukapachambue hapa vizuri hivyo umakini wa ziada unahitajika. Kabla ya kujua **kufaulu maisha ni nini** na mwalimu anaposema yule anaefanya kazi kama alivyotoa mifano hapo juu, kwamba iwe ya ualimu au upolisi kwasababu tu amekuta kuna kazi inaitwa hivyo, kwa maana yuko juu ya msingi **KAWAIDA** na amefanikiwa kujenga na kuwa na usafiri, lakini mwalimu anakwambia bado hajayafaulu maisha twende tukajifunze kitu hiki kwanza.

Mwanadarasa anaweza kujiuliza swali hili kuwa sasa nitafanya nini ambacho kweli kitakuwa cha peke yangu? Mbona kila nikitazama kwenye ubongo naona kuna kitu lakini hiki kitu tayari kinafanyika katika jamii nitakitoa wapi cha peke yangu? Kwamba hiki kitu kweli ninachokiona ni sahihi au si sahihi niendeleo kukitafuta kingine kwenye ubongo wangu??.

Hapana huenda hicho ulichokiona japokuwa tayari kinafanyika katika jamii kikawa sahihi, lakini utofauti utakuja katika namna ya **ufanyaji**, kuna vitu ambavyo tunaviita **mizizi** na wanaobahatika kuikita ardhini hii mizizi huwa katika kundi tofauti, huwa wanacho kingine cha **ziada** mbali na kuwa na kitu cha **tofauti** hawa watu kwa lugha iloyozoeleka wanaitwa (**majiniasi**), wachache wanakuwa na uwezo huo wa ziada na mara nyingi hawa ndio wanaokuja kuwa **waasisi** wa shughuli mbalimbali tunazozifanya katika jamii.

Mizizi hiyo ni nini? Katika shughuli yoyote ifanyikayo ni lazima iwe na mzizi au chimbuko, mpaka kikaitwa kilimo cha mahindi kuna aliyesababisha mpaka kikaitwa hivyo, aliyesema hiki kiitwe kilimo cha mahindi ndiye aliyekita mzizi huo ardhini, baada ya mzizi huo kuwekwa ndipo watu wengine hujaa hapo kuunda **shina**, hapa sasa kila mtu *ataangalia kwenye ubongo* wake ataona kitu tofauti na mwenzake kutoka kwenye hilo shina **walipolundikana** huku wakishikiliwa na mzizi huo.

Baadae huyu/hawa walioona kitu tofauti kutazaliwa kitu kinachoitwa **matawi**, hapa kwenye matawi ndipo mwingine ataamua kuweka tu mbegu ardhini akaenda zake kisha aje avune gunia 1, hilo ni tawi pia, mwingine ataamua kumwagilia apate gunia 10, nae ni tawi tofauti, tawi lingine litaamua kuweka mbolea apate gunia 30 na matawi mengine.

Mfano wa mzizi wa pili kuna mtu alikita ardhini mzizi wa **kufuga ng'ombe**, watu wakajua kuwa kumbe kuna kitu kinachoitwa kufuga ng'ombe, vivyo hivyo watu wengine wakaja kulundikana kwenye shina baada ya hapo kukaanza kutokeza matawi, tawi moja likienda mbali zaidi kuwa huyu ng'ombe siyo kwamba alishwe tu majani bali aongezewe pumba na mashudu pamoja na madini ili atoe lita 20 kwa siku, tawi lingine likaona kwenye ubongo wake kuwa mbona wote kwenye shina tupo kwa ajili ya maziwa? Hili tawi likienda mbali zaidi kwa kuona kuzalisha **SAMADI** ni bora zaidi nalo likawa tawi la pili na matawi mengine ambayo mwanadarasa yatakuja kichwani.

Hivyo siyo tu kwenye kilimo ama ufugaji bali nyanja zote iwe **biashara**, iwe ni **uongozi** serikalini kuna mizizi na waasisi wa hiyo mizizi na pia kuna matawi, shina huwa ni kokoro linazoa kila aina ya binadamu lakini matawi yatatofautiana, hivyo utaona tawi lingine lina rangi nzuri ya kijani huku lingine likiwa limenyauka.

Kwa maana hiyo kuona ndani ya ubongo wako kitu ambacho tayari kinafanyika kisikuogofye, ndio maana huyu jamaa anaaitwa bill gates anasema "*if you can't make it good, at least make it look good*" tutaona tawi lako linachanua vipi, je litakuwa na afya nzuri ama na afya mgogoro? Kutokana na utofauti wa kile mtu atakachokiona ndani ya ubongo wake ndicho kitakacholeta utofauti wa muonekano wa matawi.

Kuweza kuona mzizi na ukaukita ardhini hapa sasa ndipo unapovuka mipaka ya mwanajamil wa Tanzania, mwanajamil wa Afrika na kuwa katika level moja na **SUPERIOR**, usije ukachanganya siyo kila aliye nje na Tanzania, ama Afrika basi ni **SUPERIOR** la hasha yeye ni kuwa tu yuko jirani na **SUPERIOR** kuliko wewe hivyo ataiga kwa kasi kuliko wewe hivyo hata kufeli kwake kwa maisha kutakuwa na asilimia ndogo zaidi.

Mwalimu anaendelea kusema kuwa na uhakika wa kula, kulala au labda na usafiri huko siyo kufaulu maisha kwasababu mpaka uwe umeyanza kuyafaulu maisha inatakiwa ufikie ngazi ya tatu ambayo ni kuwa HAI (*being alive*), lakini unapokuwa na hivyo vitu utakuwa umeanza kuigusa kidogo ngazi ya pili ambayo ni **ISHI** (*living*) umetoka kidogo tu kwenye ngazi ya kwanza ambayo inahusisha vitu vinavyokufanya uendelee kuliona jua ngazi hii ya kwanza inayoitwa **KUWEPO** (*existing*).

Hivyo huyo mtu atakuwa kwenye kundi ambalo lina vyanzio vya kuweza kusonga mbele zaidi katika safari ya kuyafaulu maisha yake japo hatafikia akayafaulu kwa 100%

usimuulize mwalimu kwamba kwanini hapa ndipo wanafizikia wanasema "**efficiency is less than 100%**" kwanini tunaviita vyanzio kwasababu suala la nile nini halitakuwepo hivyo ataifanya REASONING yake iende kwenye mambo makubwa.

Hivyo huyu anaefanya kazi ya ualimu au polisi kama mifano ya mwalimu ilipojikita, kumiliki hivyo viliivyotajwa ni moja ya mahitaji yake ambayo kidogo yanamsogeza katika ngazi ya pili na huyu anaeweza kumudu hivi ni yule ambae ameutumia mzizi wa ualimu ama upolisi kutengeneza tawi lake na siyo yule anaefanya kwasababu amekuta kuna kitu kinaitwa hivyo au kwasababu ndo sehemu pekee iliyokuwa na nafasi au ndo sehemu pekee aliyokuwa na vigezo "**do things not by chance but by choice**" kwasababu mshahara wa laki 5 mpaka million moja utakufanya ujimudu wewe tu kitu ambacho ni kuhakikisha uwepo wako tu duniani (**existing**). Kumbuka kigezo kingine kikubwa cha dalili ya kuanza kuyafaulu maisha;

Ni kuweza kujimudu na kumudu jamii (**society**) inayokuzunguka, bila kuharibu mfumo mzima wa kuyaendesha maisha yako wewe binafsi na huitwi mtu pasipo jamii na jamii inaundwa na msingi wa neno unaoitwa mahusiano (**interrelation**) na jamii ya kwanza ni ukoo wako wewe. Ndio maana SUPERIOR anaweza kukupa msaada wewe wa kiasi chochote bila kuharibu mfumo mzima wa maisha yake binafsi.

LESSON SEVEN.

LAWAMA, HUKUMU NA MAJUTO USIYOSTAHILI.

Tuwende tukaangalie **LAWAMA NA MAJUTO USIYOSTAHILI** kama moja ya vitu usivyopaswa kuvifanya. Lakini mwalimu anaona kwanza aeleze kidogo majuto na lawama unazostahili.

Mwalimu hana shaka kuwa utakuwa unakumbuka vyema yale **makundi** mawili kama umeyasahau rejea kusoma somo lililopita Mwishoni mwa somo mwalimu alisema lawama na hukumu zinakubaliwa katika kundi la pili ambalo mwalimu alisema linahusika na kuipuuza sauti ya ndani (*inner voice*) ambapo mwili hutawaliwa na nguvu ya milango ya fahamu, ni hapa ambapo tunapata neno **tamaa** na mwalimu alimalizia kuwa hapa huhusika na masuala ya hisia kama **mapenzi**.

Mwalimu anasema katika kundi hilo la pili lawama, hukumu na majuto utakayoyapata baada ya matokeo kuja hasi hapo unastahili, kwa kukosa nidhamu juu ya ubinadamu wako na kuziheshimu tamaa, lakini hapa tutakuja kupaangalia zaidi **katika masomo yatakayohusu HISIA (EMOTIONS)** maana hatutaacha nyanja yoyote katika inayogusa maisha, na pia kukubaliwa kwa lawama hukumu na majuto haitakuwa sababu ya kufeli maisha hivyo hali hii haitakubaliwa kudumu hata ikitokea ili kuruhusu shughuli zingine ndani ya ubongo ziendelee na maisha yaendelee pia.

Na pia kama uliongozwa na sauti ya ndani kufanya kitendo chochote cha kihisia na ukapata matokeo hasi hutapaswa kujilaumu juu ya hilo ila utapaswa kutoka kwenye hilo, kwanini usijilaumu maelezo yake yataendana na mwalimu atakavyoeleza katika kundi la pili twende tukaliangalie.

Kundi la pili mwalimu alizungumzia kuwa ni kundi ambalo binadamu anajengwa katika msingi wa neno **KAWAIDA** ambapo hapa panahusisha shughuli zinazomuingizia kipato, hapa pia ataruhusiwa kujilaumu endapo amepata matokeo hasi ya shughuli yoyote kwasababu aliufwata msingi **KAWAIDA** na kuipuuza sauti ya ndani. Vivyo hivyo hali hiyo

haitatakiwa kudumu pale inakuwa imetokea ili shughuli zingine za ubongo ziendelee na maisha yaendelee.

Lakini vipi pale matokeo yatakuja hasi na wakati uliisikiliza sauti Mwalimu anakwambia usijilaumu wala kujutia wala kujihukumu kwanini twende tukajifunze na hapa ndipo msingi wa somo hili unaposimama. Kuna vitu viwili vinavyotokea katika shughuli yoyote uwe makini hapa, vitu vyenyewe ni **dhamira** au **nia** NA **matokeo**, hivi ni vitu viwili tofauti ambavyo ni lazima vitatokea katika shughuli yoyote ile. Dhamira siku zote huwa na upande mmoja yaani huwa **CHANYA** lakini matokeao huwa na pande mbili **HASI NA CHANYA** hivyo lazima matokeo yataegemea upande mmoja, tutajikita zaidi kwenye upande **HASI** maana huku ndiko kwenye lawama, majuto na hukumu juu yako mwenyewe.

Hupaswi kujilaumu, kujihukumu wala kujijutia kwa matokeo hasi kwa sababu kwa binadamu yeyote mwenye akili timamu ni lazima atakuwa na **DHAMIRA** njema kabla ya kutekeleza shughuli yoyote hivyo usijilaumu kwasababu ya matokeo ndio maana kama wewe ni mkulima uliwahi kila siku saa kumi na moja kwenda shamba ukashinda huko mpaka jua lilipozama, pengine ukashinda hata na njaa. kama wewe ni mfanyabiashara pengine ulitembea umbali mrefu kufuata bidhaa zako pengine ulitukanwa hata na wateja wako lakini bado ulifanya kwa moyo mmoja.

Ulifanya hayo yote kwasababu ya **DHAMIRA** iliyokuwa njema lakini mavuno yanapokosekana shambani au hasara yoyote inapotekea katika biashara siyo sababu ya kujilaumu wala kujihukumu, kwasababu kwa kila shughuli unayopanga kuianza kabla ya kuifanya hauwezi ukapanga kuja kupata matokeo hasi.

Hivyo dhamira itabaki lengo kuu na matokeo yatabaki kama matokeo hivyo kwa matokeo hasi yanakuja ili kuboeresha ufahamu wako hivyo hatuna neno **KUFELI** pale matokeo yanapokuja hasi ila tuna maneno haya "**Njia ambazo hazijaleta matokeo sahihi kulingana na dhamira**" hivyo inakuhitaji ubadili njia na kubadili njia kunawezekana tu endapo akili yako haitakuwa na hatia juu yako hivyo kuupa ubongo wako nguvu ya kusukuma akili nyingi ili kuleta njia zingine bora.

Hivyo ndivyo ubize wa **SUPERIOR** unavyokuwa bize ni katika kutafuta njia bora wakati ubongo wa wewe mwingine huku unakuwa bize kwenye kujutia na kujihukumu, **homework** kwako mwanadarasa unafikiri ni nani ataendelea kusonga mbele kati ya hawa

watu wawili anaetafuta njia na anaejihukumu?. Kuna huyu jamaa anaitwa THOMAS EDSON mgunduzi wa bulbu anasema, katika jaribio lake la ugunduzi wa bulbu SIKUFELI MARA elfu kumi ila nilitumia NJIA elfu kumi ambazo hazikunipa majibu sahihi katika ugunduzi wa bulbu. Hivyo kataa neno kufeli itoe akili mahakamani songa mbele.

LESSON EIGHT

FANYA MAAMUZI SAHIHI NA SIYO MAAMUZI YA KUPENDEZA.

Kuna misingi miwili msingi wa **KUPENDA** na msingi wa **KUWEZA**. Maamuzi yanayotokana na msingi wa **KUWEZA** huwa ni **SAHIHI** lakini maamuzi yanayochipukia kwenye msingi wa **KUPENDA** huwa 90% si sahihi na wanadarasa wengi wako hapa na huu ndo msingi unaokuwa wa kupendeza matokeo yake mwanadarasa anaenda kaskazini huku mafanikio yakienda kusini.

Moja ya kosa kubwa ambalo wanadarasa walio wengi hulifanya ni kushindwa kutofautisha maneno haya mawili **KUPENDA** na **KUWEZA** katika kuwaongoza kufanya maamuzi juu ya shughuli gani watakayoifanya itakayowaingizia kipato. Ni 10% tu ya watu ambao hufanikiwa kwa kuanza na msingi wa maamuzi wa **KUPENDA** kwa maana nyingine ni 10% tu ya wale wanaofanya shughuli fulani kwasababu wanaipenda na wakajikuta ndiyo shughuli haswa wanayoiweza lakini 90% ya watu hawafanikiwi kwasababu licha ya **KUPENDA** kwao huwa hawawezi.

Lakini watu wanaofanya shughuli fulani ya kuwaingizia kipato kwa kufuata msingi wa maamuzi wa **KUWEZA** ni 80% wanaofanikiwa pasipo kujalisha kama hicho kitu walikuwa wanakipenda au laah. Kwanini 80% hii ni kwasababu **KUPENDA** na **KUWEZA** ni maneno ambayo yamezaliwa kutoka katika nyanja mbili tofauti, tukianza na **KUWEZA** hili limetokana na chimbuko la uumbaji au uweza aliopewa binadamu ndani yake, na ni tofauti na aliopewa binadamu mwingine, lakini neno **KUPENDA** linatoka katika nyanja ya **HISIA** hivyo ni kitu kinachoweza kujengwa au kubomolewa wakati wowote.

Baada ya watu kuanza kufanya shughuli fulani kwa maamuzi ya **KUWEZA** huwa wanaanza na kutokuipenda hiyo shughuli lakini kwasababu **KUPENDA** ni kitu cha **HISIA** huanza kujijenga na kisha mtu huanza kuipenda hiyo shughuli, tofauti na aliyeanza **KUPENDA** hataweza kufanikiwa kwasababu kuweza hakuji njiani sio kitu cha hisia bali ni kitu cha uweza. Hivyo huyo mtu hatafanikiwa kwasababu ataishia kuiga jinsi ya kukifanya kitu hicho kwa kuwa hana uwezo nacho.

20% zinaenda wapi kwa watu wanaoanza na msingi wa **KUWEZA**? hawa wanashindwa kufanikiwa kwasababu hushindwa kukuza hisia za **KUPENDA** wanachokiweza hivyo huwa ngumu kufanikiwa kwa asilimia zote, kwasababu watafanya pasipo uhuru wa akili na nafsi na pia watafanya chini ya uwezo wao kwa kukosa **ARI** ya kukifanya hicho kitu. Hivyo tuna mifumo miwili ambayo ni;

1. **KUWEZA**---> **KUPENDA** hapa ndipo mtu atakapofanya kitu kwanza kwasababu anakiweza kisha kupenda kutajijenga baadae kwasababu hisia hujengeka katika pande mbili furaha na huzuni hivyo hisia ya kupenda itakuja kutokana na furaha ya mafanikio.

2. **KUPENDA**--->**KUWEZA** huu mfumo wa pili 10% tu ndio watakao fanikiwa na hiyo itatokea endapo mtu pamoja na kuamua kukifanya kitu kwa kukipenda lakini ni kitu ambacho ndicho alichona uwezo nacho, 90% hatafanikiwa kwasababu hawatakuwa na uwezo nacho hivyo wataishia kuiga.

Msingi wa **KUWEZA** mara nyingi hupuuza kwasababu mara nyingi kile mtu anachokiweza kinakuwa hakimpendezi machoni pake au hakimpendezi machoni pa wanajamii, Hivyo hakitamfanya aheshimike au kitamfanya jamii imdharau hivyo atakikwepa na kwenda kung'ang'aniza kile anachokipenda, kwasababu 100% ni lazima atakipenda kitu chenye taswira nzuri mbele yake na jamii kiujumla. Mwanadarasa unaweza kujiona wewe ni mtanashati ama mrembo hivyo kuuza juice au matunda kutakufanya usiheshimike mbele ya jamii na kukushushia hadhi lakini ni kitu ambacho **UNAKIWEZA** kwa 100%, yani ukiongea tu mteja kesho atakuja tena kwasababu uweza wako umejengeka katika kauli.

Inawezekana umejengwa uweza ndani yako ukamfundisha au kumwelekeza mtu mpaka akaelimika lakini kwasababu tu hutaki ualimu basi hautakuwa tayari kukifanya hicho kitu huku uking'ang'aniza kuwa mfanyakazi wa benki kwasababu hata jamii ikikuona kuwa upo sehemu ya kiyoyozi itasema ndiyo yule, ndiyo ni mtu fulani, lakini kuwa mwalimu kama *mwalimu wako* hapa jamii itakudharau.

Na hii misingi ndiyo ambayo hujengwa mpaka kwa watoto wetu na hivyo kuwaelekeza katika mwelekeo wa vitu vinavyoonekana na wanajamii vyenye kupendeza sana, Lakini tunasahau msingi wa kuwaelekeza watoto wetu katika mwelekeo wa vitu wanavyoviweza. Mwanadarasa utakuwa shahidi hapa pale inapoinuka misemo kama;

1. "Napenda sana kufanya hiki lakini sifanikiwi nimetumia nguvu na akili yote lakini wapi" mwalimu anakwambia hapo akili haitumiki bali kivuli cha akili, ubongo hauwezi kusukuma akili ikafanye kitu ambacho hauna uwezo nacho, hapa utatumia akili inayotokana na nguvu ya macho kwa kuiga kile unachokiona.

2. "Sipendi kufundisha" lakini matokeo kila yanapokuja somo lake ndilo ambalo la kwanza kufaulisha au wanafunzi wanajivunia kuwa nae kwasababu wanamwelewa" hapa ni pale unaposhindwa **KUPENDA** unachokiweza.

Msaada wa ASILIA (nature).

Asilia au nature kama wengi wanavyoelewa kwa urahisi husaidia sana kumlazimisha mtu arudi afanye kile anachokiweza, hapa ni pale kauli hii hutokea "*Nilikuwa najaribu tu kufanya hivi lakini nimefanikiwa hata siamini nahisi nimebahatisha*" hapo mwalimu anakuambia umeongozwa na nature kukusaidia kukuonesha kile unachokiweza ili uache kuhangaika na kile usichokuwa na uwezo nacho, lakini mtu hataendelea kukifanya kitu hicho kwa ufanisi zaidi akiamini ni amebahatisha.

Hivyo mwalimu anakwambia mwanadarasa fanya kitu unachokiweza, **KUKIPENDA** kutakuja tu kwasababu kupenda ni **HISIA**, utakapofanya unachokiweza ndipo ambapo ubongo utasukuma akili nyingi zaidi na kukuonesha kile ambacho wengine hawakioni juu ya shughuli hiyo. Haijalishi hicho kitu unachokiweza hakina heshima sana mtaani au hakina heshima mbele ya macho yako lakini amini wewe ndiye utakaeenda kubadilisha taswira nzima ya hiyo shughuli na kuifanya iheshimike mbele ya jamii.

Usiende kuimba kwasababu Unapenda muziki nenda kwasababu unaweza muziki, Usifanye kitu kwasababu ya jina lake ambalo lilijengwa na watu waliokuwa wameumbwa na uwezo wa kukifanya hicho kitu, bali fanya kwasababu unaweza hatakama ni kitu chenye hadhi ndogo, kuna huyu jamaa anaitwa **Napoleon Hill** anakwambia "*do small things in a great way*"

Pia wewe umechelewa kukifanya unachokiweza mwanao hajachelewa tutakuja kuchambua vizuri tukifika katika chapisho linalozungumzia Elimu hii iliyoko mtaani kwako mwanadarasa hivyo usije Ukashangaa Ronaldo pamoja na kuwa na hela nyingi za kuweza kumpeleka mtoto wake shule yoyote ile hata ikianzishwa sayari nyingine Lakini atampeleka Akademiki ya mpira kwasababu anampeleka kwenye kitu ambacho mtoto anaweza.

LESSON NINE.

NJIA ZA KUSAFISHA UBONGO NA AKILI.

Njia ya kwanza

Samehe kizazi kilichopita.

Hapa tunazungumzia nini, ni pale mtu anapata unyonge wa nafsi kutokana na familia iliyomleta duniani, kwa kushindwa kumuandalia mazingira thabiti ambayo yangemfanya asiwe hivyo alivyo. Anajiona alikuwa na uwezo mkubwa wa kuelewa masomo shuleni lakini kutokana na hali duni ya wale waliomleta akakosa kwenda shule nzuri ambayo leo ingemfanya aonekane mtu fulani katika jamii.

Anajiona ana uwezo mkubwa wa kufanya biashara lakini kutokana na hali duni ya wale waliomleta anakosa msaada wa kuwezesha hata kupata mtaji. Kijimshahara anachokipata hakimtotherezi lakini ni lazima apate usumbufu wa kuombwa na hata kusaidia bila kuombwa kwasababu nayeye anaona hali ya uduni iliyopo.

Anaishia kulaumu nafsi yake, anaona **HATIA** iliyoambatana na huruma juu ya kizazi chake kilichopita *kwa maana ni kweli lilikuwa jukumu la waliomleta duniani kumwandalia mazingira*. Hasira ndani ya moyo wake inamjia akiona fursa zilizowazunguka waliomtangulia lakini walishindwa kuzifanyia kazi. Anapata **WIVU** ndani yake unaojawa na hofu ya kuogopa kukufuru, wivu huo ukimwachia kauli ya kwamba **"Mimi ndio ningeza iliwa familia ile"**.

Mwalimu anakwambia kuja kwako wewe duniani siyo ili ufanane na waliokuleta bali ulete kitu kipya, muda mwingi unaotumia kuwaza na kunung'unika na kujiona si mwenye bahati **NDIO** kitu kitakachokufanya uje ufanane na waliokuleta kisha hali hii iendelee kwa kizazi utakachokijenga wewe. Mwalimu anakwambia jione mwenye bahati kwasababu wewe ndiye unayeenda kufanya **NURU** ndani ya kiza nene, ndiyo maana umeweza kuyaona haya.

Waliokutangulia hawakuyaona haya hivyo pamoja na fursa walizozikuta upofu wa kuziona uliwaandama, kumbuka msemu unaosema kuwa *"minds are like parachutes, they function only when open"*. Ona Fahari kwasababu wewe unaenda kuwafungua

UBONGO wanaokuzunguka, ni Fahari kubwa pale unapokuwa MWANZILISHI wa mapinduzi yenye tija kuliko pale unapokuwa MWENDELEZAJI.

Epuka maneno yafutayo;

Epuka kutumia dini kama kigezo cha faraja ya hali duni uliyopo. Kuna msembo wa huyu jamaa anaeitwa **karl Marx** anasema "*Religion is the impotence of human mind to deal with occurrences it cannot understand*" mwalimu anakwambia kama hali duni ingekuwa ndiyo njia ya kuitukuza dini yako basi ungelikuwa sahihi lakini hata yule aliyekuletea hicho unachokiamini hana hali kama uliyonayo.

kulingana na imani yako dini ikusaidie wewe kuja kukufikia kule unakoamini kuwa kuna maisha mengine baada ya kifo, kuliko ukishike hicho unachokiamini ili uweze kula, *hahaha!* Unaweza ukaishia kufanikisha kula na usifike unakoamini kuwa kupo. Umepewa akili na utashi maarifa na ufahamu vifanyie kazi.

Pia kumbuka **bill gates** anakwambia "*kuzaliwa maskini siyo kosa lako bali kufa maskini*" Hii ni njia ya kwanza ya kusafisha UBONGO na AKILI bado njia mbili.

Njia ya pili

Jisamehe mwenyewe.

Moja ya mzigo mzito ambao moyo, nafsi na ubongo wako unabeba ni HUKUMU ya **ndani** inayokupelekea ujione mwenye **HATIA** juu ya hali ya maisha uliyonayo na juu ya hali ya maisha uliyopitia. Na tena kabla ya kuzama ndani zaidi anza kwa **kujisamehe** kwa kutokuijua elimu hii, mwingine atajilaumu kwanini asingeyasoma yote haya kungali mapema. Mwalimu anakwambia huu ndio muda wako muafaka wa wewe kuyajua haya, kama haitakuwa juu ya faida yako basi itakuwa juu ya jamii yako inayokuzunguka.

Kuna huyu mzee mwenzangu anasema; "*forgive yourself for not knowing what you don't know before you learned it*" Hivyo usijihukumu kwa hili pia.

Kujiona mwenye hatia juu ya hali ulizopitia katika maisha yako kunakuja baada ya mengi uliyoyafanya na matokeo yake yakawa ndivyo sivyoyawaza jinsi ulivyoianza biashara flani lakini mwisho wa siku ukaporomoka mpaka kuja kula mtaji na sasa umebaki hauna kitu, sura inaonesha tabasamu mchana lakini usiku ukizima taa basi unayawasha

mawazo mpaka asubuhi huku swali kichwani likiwa kwanini sikufanya vile? Kwanini sikutumia njia ile?

Huku unasahau kuwa kabla ya kufanya ile biashara ulikuwa na dhamira njema, ukiomba kabisa na Mungu akusaidie uweze kuinuka katika maisha kupitia biashara ile, lakini ukasahau jambo moja kuwa **DHAMIRA** na **MATOKEO** ni vitu viwili tofauti, unatamani siku zirudi nyuma uanze upya, unaishia kujitupia lawama za kuona matokeo uliyoyapata ni **UZEMBE**.

Mwalimu anakuweka sawa juu ya neno **uzembe**, ni pale unapofanya jambo unalolielewa vyema bila ufasaha wake, kwa mfano najua kabisa ili niweze kuvuna mazao yanipasa kuweka mbolea ya kukuzia lakini endapo sitaiweka, siku nikija kupata mazao hafifu kwasababu sikuweka hiyo mbolea ni **UZEMBE** haijalishi nilishindwa kuweka kwasababu gani.

Tofauti na hapa mwanadarasa anapojiona mzembe kwa kitu ambacho alitumia akili yake yote, maarifa ufahamu na nguvu zake zote katika kufanya kitu hicho, lakini kikaja kuleta majibu **HASI** huo sio uzembe bali ndipo **UBONGO** wako ulipoishia kusukuma kiwango cha akili iliyotumika katika kutekeleza kitu hicho. Hivyo hupaswi kujihukumu na kujiona mwenye hatia kwa kitu ambacho ulikifanya kwa **DHAMIRA** nzuri halafu kikaleta majibu hasi.

Nini ambacho ulitakiwa kukifanya ni hiki, kuna Dr mmoja anaitwa **Dr.Seuss** anasema “*Don’t cry because it’s over, but smile because it happened*” usilie kwasababu unaona ndo mwisho, mambo yote yameharibika laah hasha bali tabasamu kwasababu tayari yamekwishatokea.

Kuna njia mbili za kujifunza

Njia ya kwanza kwa **kuona**, kwa kuuliza, kwa kuelekezwa, kwa kusikia na kwa kila aina ya kutumia milango yako ya fahamu ikiwa na maana yote ya kujifunza kitu kwa kupata usaidizi wa nje (**external support**).

Njia ya pili na ndo njia iliyobora na ndo njia inayokuja kuletea hukumu na hatia ndani yako nayo ni njia ya **JARIBIO**, njia hii inahusisha “uhusika wa wewe mwenyewe katika kutekeleza kujifunza” na kupata msaada mdogo kutoka nje hapa ndipo ambapo mtu anapoingia kwenye biashara kama ni ya nguo atakachohitaji msaada ni kuelekezwa kuwa sehemu gani atapata nguo za jumla lakini shughuli zingine zote zinazofuata zinakuwa juu

yake, yeye ndio atajua nguo hii nilinunua elfu kumi hivyo mimi niuze elfu 15. kwanini tunaita jaribio ni kwasababu kitu chochote unapokifanya kwa mara ya kwanza kinakuwa ni jaribio.

Kwamba una nadharia kichwani kwamba hiki kitu kinaenda hivi na hivi wana kemia wanaita (**hypothesis formulation**) lakini je ni kiko hivyo? Hivyo kukifanya ndo jaribio lenyewe ambapo utakuja kujua kama uko sahihi au hapana. Sasa basi **kuwa makini hapa** matokeo yoyote ya **jaribio** lako huwa ni njia ya kujifunza haijalishi matokeo ni mabaya ama mazuri, hapa ndipo unapokuja kujifunza kwa kitu tunachoita **UZOEFU (experience)**.

Tatizo la wewe mwanadarasa endapo matokeo yatakuja mabaya basi huwa ndo mwisho wa safari, mwalimu anakwambia hilo ndo kosa kubwa, yani unaacha kitu baada ya kukijua, unapata hofu ya kukifanya tena baada ya kukijua na huku ulikifanya kwa ujasiri kabla ya kukijua *inachekesha sana*. Ndio maana katika kujutia kwako au kujilaumu kwako unazungukwa na mawazo ya kwanini nimefanya hivi na kwanini sikufanya vile lakini unasahau kuwa umezijua njia hizo kwasababu yametokea.

Unapishana na mavuno mwanadarasa, nini unatakiwa kufanya msikilize huyu jamaa anaeitwa **Joseph Campbell** anasema “**we must let go of the life we have planned, so as to accept the one that was waiting for us**” tayaruhusu yale matokeo yetu yaliyotupata, tuyaache yaende maana yale ndiyo tuliyokuwa tumejipangia lakini kuna uhalisia wa jambo ambao ulikuwa unatusubiri lakini ulituhitaji tungali tumejifunza tayari. Sio huyo tu kuna huyu jamaa mwingine anaeitwa **Thomas A. Edson** mgunduzi wetu wa bulb anasema;

“Our greatest weakness lies in giving up, the most certain way to succeed is always just to try one more time” udhaifu wetu mkubwa ni kukubali kushindwa lakini njia ya mafanikio pasi na shaka ni kujaribu kwa mara nyingine tena.

Mwalimu anakwambia usijione mwenye hatia wala kujihukumu **jisamehe** jione uko huru akili ipate uhuru wa kuwaza njia bora ambazo ni zaidi ya zile ulizokwishazitumia. Kuendelea kujiona mwenye hatia ni kuzidi kupunguza muda wa akili nyingi kuelekezwa kwenye ufumbuzi kwasababu majuto sio tiba hata hivyo.

Njia ya tatu

wasamehe wanaokuzunguka.

Mwalimu anaposema wanaokuzunguka, hamaanishi majirani zako tu hapo nyumbani kwako/kwenu, bali watu wote ambao wanahusika moja kwa moja katika maisha yako. Kuanzia ndani ya familia yako, mahali unapoishi, kazini kwako, na Tanzania kwa ujumla mpaka hata dunia kwa ujumla kama una watu wanaokujua huko.

Ndani ya familia yako kunapokucha siku nyingine una majukumu fulani ni sehemu ya maisha yako, ukitoka nje utasalimiana na majirani (**degree of socialisation**) tayari ni sehemu ya maisha, Utanyanyua simu kuwasiliana na mtu ambaye yuko mkoa mwingine au nchi nyingine nao ni sehemu ya maisha yako ni watu wanaokuzunguka.

Watu hawa wanaokuzunguka ni lazima wawe na uhusika wa moja kwa moja katika maisha yako, ni lazima ushirikiane na binadamu mwenzi ili kukamilisha maisha yako. Sasa katika kukamilisha huku maisha yako kwa uhusika wa binadamu mwenzi kutaambatana na matokeo mawili **HASI** na **CHANYA**.

Wapo ambao uhusika wao utakuletea matokeo **CHANYA** katika harakati za kuendesha maisha yako, hawa hatuna shida nao kwasababu hauwezi kuwa na kinyongo na mtu anaekuletea matokeo chanya. **HAWA** hatutawazungumzia kwasababu hawahitaji msamaha wowote.

Kwenye kundi hili lingine ambalo uhusika wao katika maisha yako unaleta matokeo **HASI**, hawa ndio walengwa haswa, hawa ndio ambao tunakinyongo nao kwa kuona pengine ugumu wa maisha tunaopitia umechangiwa/kusababishwa na wao. Hapa tunaongelea uhusika ulio ndani ya ubinadamu na si **ZAIDI/NJE** ya uwezo wa kibinadamu (**beyond human capacity**).

Tunapozungumzia uhusika wa zaidi/nje ya uwezo wa kibinadamu ni pale mtu anapoamini kukwama kwake au hali aliyonayo katika maisha ni kwasababu ya **“KUROGWA”** huku mwalimu hataongelea kwasababu huku kunasimamia katika msingi wa **IMANI** ya mtu.

Tukija kwenye uhusika wa ndani ya uwezo wa binadamu kumegawanyika katika makundi mawili, la kwanza;

Uhusika wa kiumbo.

Uhusika huu wa kiumbo ni pale mtu anapofanya jambo ambalo **linaonekana** na moja kwa moja linaathiri sehemu ya maisha yako au linakuletea matokeo hasi katika maisha yako.

Kwa mfano mtu uliyekuwa unamtumia kwenye biashara zako kaingiza hasara kwa kutapeliwa, unafanya kazi fulani wafanyakazi wako wamefanya kazi chini ya kiwango na kusababisha kutofikia lengo fulani, Umelima mifugo ya jirani yako imeingia shamba na kula mazao, wafanyakazi wenzako wanakuongelea vibaya kwa boss wako mpaka ikafikia boss kakusimamisha kazi, kuna hela uliziweka ndani mtoto wa mjomba wako ambae unaishi nae kakuibia, na mambo mengine mengi ambayo mwanadarasa umeyashuhudia au kufanyiwa na watu wanaokuzunguka yakakuletea matokeo hasi ya moja kwa moja ambayo yamepelekea kuwa na hali fulani katika maisha yako.

Mwalimu anaenda kukufundisha jinsi ya kupambana na uhusika huo, uwe makini hapa.

Unaenda kupambana kwa njia ya saikolojia (**psychology**). Twende ukajifunze.

Moja ya kosa ambalo watu wanalifanya baada ya kutendewa jambo lililoleta matokeo hasi ni kutaka kulipa **KISASI** kwa mtenda. Mwalimu anakwambia Kisasi hakijawahi kuwa **SULUHU** na wala hakijawahi kuwa njia ya kukufanya mtendwa ukapata **AMANI** ndani ya moyo wako, mwanadarasa unabeba mizigo ndani ya moyo ambayo inakumaliza na kukuua na kukuwekea giza la kushindwa kuwaza nje ya zile 20%.

Kwanini kisasi hakijawahi kuleta **AMANI** ni kwasababu kabla ya kukitekeleza unakuwa na mzigo unaoitwa **KINYONGO** na kinyongo kinakuja kwasababu **HAUJASAMEHE** hivyo hata baada ya kutekeleza kisasi chako hautautua huo mzigo wa kinyongo kwasababu hakuna kisasi kinachokuwa kwenye mzani sawa na kinyongo, na hata yule unaemfanyia kisasi hautamfanya akuone wewe ni mwamba bali atatafuta njia ya kukufanyia kingine cha kukuumiza kwasababu asili ya binadamu imeumbwa kwa **KUTOKUBALI** kushindwa kwa jambo lolote lenye kuumiza.

Asili ya binadamu inamruhusu binadamu kukubali kushindwa kwa jambo la furaha **hahaha** hapa ndipo panapomchekesha mwalimu, binadamu anaweza kukubali

kushindwa katika kufanya shughuli fulani ambayo ingemletea mafanikio ambayo yangemletea furaha, lakini hakuna binadamu anaekubali kushindwa kwenye jambo linalomuumiza kwa mfano mtu akipata ugonjwa atapambana na tiba zote hatokubali kushindwa mpaka dakika ya mwisho anapotokwa na roho, hivyo ndivyo asili yake (**nature**) ilivyo.

Hivyo hautafanya **SULUHU** kwa kisasi kwasababu ni kitu cha kuumiza hivyo mtenda hataishia kukubali kupokea kisasi chako bali atakuja tena kwa njia nyingine kama siyo leo basi kesho, kama siyo mwaka huu basi ni mwaka ujao na kama siyo yeye basi atakuja kufanya mwanae na kama siyo kwako basi hata kwa kizazi chako, na ndio sababu ya kauli hii kuja “Sio mara ya kwanza kwa yeye kunifanyia hivi mara ya kwanza alivyonifanyia nilimfanyia vile lakini bado hakomi sijui ananitafutia nini”.

Hivyo mwalimu anataka kukufundisha kitu cha tofauti cha kupambana na uhusika wa aina hiyo, ambao amesema unapambana kwa kutumia saikolojia (**psychology**). Unapambana na kitu kinachoonekana kwa njia isiyoonekana, Kwanini, mwalimu anataka kukufundisha njia isiyoonekana kwasababu kila unachokiona kimefanyika kilianza kwanza kwa kutokuonekana, mtu kabla ya kukuibia aliwaza kwanza, mtu kabla ya kukuchongea kwa boss wako alikuwazia upande hasi kwanza, mfanyakazi wako alipofanya kosa fulani katika biashara kwa makusudi au laah bado aliwaza kwanza kwamba **NGOJA** nifanye hivi.

Hivyo tunaenda kupambana kwanza na mzizi wa tukio na si matokeo ya tukio. Njia nyingi zilizozoeleka hazina ufumbuzi wa matatizo na ndio maana matukio yanajirudia katika jamii, nenda sambamba na mwalimu utajifunza mengi, siyo tu utofauti wa kufanya shughuli fulani ili ikuingizie kipato kizuri, bali pia utofauti wa kukabiliana na haya, unaweza ukafanya shughuli yoyote kwa utofauti na upekee mkubwa lakini usione mafanikio kwasababu ya kutoyajua haya.

Tutaanza kwa hatua kadhaa katika kutumia njia isiyoonekana.

Kwanza kabisa yanapotokea matukio hasi kabla ya kufanya chochote, kaa chini chukua dayari (diary) yako andika pembeni hilo tukio linakuletea funzo gani, umeibiwa na wanafamilia Nyumbani kwako kwasababu labda ni mgumu wa kutoa hela lakini unazo, labda kwasababu haujaweka usalama wa kutosha sehemu unapohifadhi vitu nyeti. Shamba lako mifugo imeingia na kula mazao labda sababu haujaweka mwangalizi wa shamba au

labda haujazungushia wigo shamba lako na unajua sehemu uliyopo pana mchanganyiko wa wakulima na wafugaji, kijana wako kafanya kazi chini ya kiwango labda ni kwasababu hautoi semina elekezi. Hivyo jambo lolote linapotokea ni funzo kwanza. Baada ya hatua hiyo unaenda kufanya kitu cha kisaikolojia ambacho mtenda kitamsumbua sana na huku hamna kisasi patamu hapo;

Mwalimu anakunywa glass ya maji kisha anacheka kidogo na kusema *“hakuna kazi ambayo ingekuwa inachosha na kuboia kama kula na kunywa kama Mungu asingeumba vitendo hivyo kuwa vya starehe”*, mwalimu anaona kwanini Mungu hakukiumbia starehe kitendo cha kusoma watu wengi wangepadilika na jamii kiujumla maana hamna mabadiliko ya kweli kama mabadiliko ya kichwani kwenye ubongo tutakuwa tunapiga kelele tu kutaka kubadili tabia za watu pasipokuanza na kichwani. *“human can alter their lives only by altering their attitudes of minds”* by William James.

Turudi kwenye somo bado tupo kwenye uhusika wa kiumbo, kama umepasahau hapo rejea kusoma hapo juu, tunaenda kupambana sasa na mtenda kwa kutumia njia ya kisaikolojia kama hatua ya pili, lakini kabla ya kuzama hapo kwa kina kabisa mwalimu anataka kukuweka sawa juu ya hawa wahusika wanaokuzunguka, ni hivi tunaongelea wahusika wanaokuzunguka unaoshirikiana nao ambao mlikuwa mnaishi kwa amani kabla ya kukuletea matokeo **HASI** hivyo usichanganye na **AJALI**, mfano wa ajali ni kama jambazi huyo si mshirika wako labda mwizi wa mtaani tofauti na vile atakavyokuibia mwanao ndani ambae huwezi mfunga jela.

Hao watu wanaoleta matukio hasi tunaowaita ajali hawahusiki katika njia hii ya kupambana kwa kutumia saikolojia hawa wanahitaji **NGUVU** lakini si ilimradi nguvu kuna somo tutakuja jifunza linaitwa hivyo, hapa tunaopambana nao walengwa haswa ni wale tunaoshirikiana nao katika shughuli za kutuingizia kipato, au shughuli yoyote inayotupatia mahitaji muhimu yanayofanya tuzidi kuamka tena na tena kama kilimo, biashara na kadhalika.

Mwalimu ataenda kutupa story moja ilimtokea mwenyewe miaka hiyo angali kijana. Umri wa Mwalimu umemfanya ayashuhudie mengi. Stori ya kwanza inayomuhusu mwalimu mwenyewe kipindi angali kijana inanza hivi.

Kipindi mimi mwalimu **FARADAY** nipo kidato cha tano shule ya bweni miaka hiyo, nilitoroka na kwenda mjini kusafisha macho kidogo, kutokana na shule yenyewe ilikuwa mbali na mji kidogo, basi mimi huyu **FARADAY** nikaendelea kupuyanga na mtaa huku na huku, huku na huku mara secondmaster wa shule huyu tukagongana ana kwa ana, ikawa hamna namna tena ikabidi kusarenda na kizuri zaidi tulikuwa na mwenzangu basi ilibidi tushiriki kiama chetu. Alichokifanya yule second master ni kutubeba kwenye pikipiki yake akaturudisha shule na tulipofika shule akaturuhusu tuende mabwenini bila kuongea chochote.

Kilichofwata “*kuwa makini hapa mwanadarasa*” akili yangu mimi Faraday na mwenzangu tulijua kesho mstarini lazima makalio yetu yachezee bakora kama ilivyokuwa desturi ya mwalimu huyo, kamwili ka mwalimu Faraday kwa wakati huo hata avae suruali nne kwa wakati mmoja huwezi kuona tofauti basi mimi na mwenzangu tukatupia suruali aina ya jinsi ndani tukawa tumenenepa miguuni tu basi kama ilivoda siku ikafika second master akaja mstarini alichokifanya ni alitangaza tu matangazo mengine akaenda zake.

Basi tukatoka wanyonge tukishiriki kesho tena tukajua leo pengine anawahi vikao siku ya pili ikawadia alikuwa amesafiri kwa siku mbili, tukapumua kidogo huku tukijua akirudi anaanza na sisi lakini alivyorudi akatoa matangazo machache akaenda zake tukajua labda ni kwasababu ya uchovu wa safari siku iliyofwata tukajitupia suruali za kutosha lakini hakuja kabisa basi ikawa hivyo tuliteseka kwa wiki mbili mwisho tukakata tamaa kwamba basi tushiriki pale siku akiamua tutaadhibiwa.

Yule mwalimu hakutupiga wala kutuuliza mpaka tunahitimu shule lakini tuliishi kwa muda mrefu tukimkwepa kwa kuhofia akituona tu atakumbuka, kwamba labda alikuwa amesahau, ilifikia mahali tukataka twende tukajipeleke wenyewe tumuombe atuadhibu ili yaishe lakini tukasita.

Tunarudi kwenye somo letu, kumbe mwalimu alikuwa ametusamehe lakini akawa ametupa Adhabu iliyotutesa kwa muda mrefu, alijua akili ndiyo iliyotutuma tutoroke hivyo akaamua kuiadhibu akili yenyewe. **Hatukurudia** kutoroka tena na hatukuthubutu kumuudhi tena yule mwalimu kwa kuhofia angekumbushia na siku ile. Hivyo yeye alisamehe akafuta kinyongo ndani mwake akatuadhibu kisaikolojia tukapata adhabu ya muda mrefu na hatukuwahi kujenga kisasi chochote juu ya huyo mwalimu na pia wakati anatupakia kwenye

pikipiki alituuliza tumefwata kununua nini tukamuonesha kuwa tuliishiwa nguo za ndani baada ya siku kadhaa duka letu la shule wakawa wanauza makufuli ya kiume, **hivyo mwalimu alipata funzo kwanza lililotokana na kutoroka kwetu.**

Naamini kupitia story hiyo mwanadarasa umeanza kupata mwanga. Hivyo tukio lolote linapotokea lina kitu cha kujifunza. Tutatumia story hiyo moja kama mfano.

Chanzo cha matukio mengi kutoka kwa watu wanaotuzunguka ni tabia lakini chanzo cha tabia huwa ni ndani tabia inazilishwa na vitu vitatu, matamano, hisia na maarifa kuna huyu jamaa **plato** anasema “**human behaviour flows from three sources, desire, emotions and knowledge**” hivyo kuhangaika kuzuia tabia ya mtu ni kutwanga maji kwenye kinu, inabidi kuzuia chanzo cha tabia, leo hii ndio maana makosa yanajirudia kwasababu watu wanazuia tabia na si chanzo cha tabia. Hamna mtoto unaemzaa akawa mwizi toka tumboni, hamna mfanyakazi aliyesomea kitu Fulani ili aje afanye uzembe hapana.

Leo hii inawezekana umeajiri mpaka sasa idadi inafika wafanyakazi wanne kwenye kitengo kimoja wale watatu wote wa mwanzo umewafukuza kwa kukuletea matokeo hasi bado haujafanya suluhisho hata huyu aliyepo atafanya nae utamfukuza, watu wamekuwa wakiwafumania wenza wao na kutoa talaka lakini wanakuta mwanamke mpya nae kafanya yaleyale utafukuza mpaka uzeeni **hahaha** somo hili linampa raha sana mwalimu.

Jinsi ya kutumia hii njia isiyoonekana katika kupambana na wahusika, mwalimu anakwambia usipambane na wahusika kwa njia zilizozoeleka kwasababu si sahihi na kama zingekuwa sahihi basi makosa yasingejirudia. Kupambana unakoenda kukufanya hapa ni kupambana na ubongo wa mtenda ambapo utaenda kumpa mshtuko mkubwa ndani yake.

Mwalimu anakwambia kwa kosa lolote ambalo umefanyiwa na mtu anaekuzunguka kitu cha kwanza usifanye kile ambacho yeye mtenda anategemea utamfanyia kwa mfano Leo mfanyakazi wako kasababisha hasara yeye tayari anakuwa amekwisha jihukumu kuwa hapa nafukuzwa kazi hivyo hata ukimfukuza kazi hakitakuwa kitu kigeni nafsini mwake.

Leo hii mifugo ya mtu ikila shambani kwako ukaipeleka mifugo hiyo ofisi ya kijiji na mwenye mifugo akalipishwa faini halitakuwa jambo la kumshtua, Leo hii ukimfumania mwenza wako kisha ukamtimua au ukampa talaka ni kitu ambacho alijua kitatokea endapo

utagundua. Hivyo unapopambana na muhusika huyo kwa njia zilizozoeleka unakuwa unatekeleza kitu ambacho sauti yake ilimkataza lakini kwasababu aliipuuza hivyo hataweza kubadili tabia kwasababu baada ya kuipuuza sauti yake ya ndani alivyofikiria matokeo hasi ya kile alichenda kukifanya alikiundia njia za kukabiliana nacho.

Hivyo pale muhusika anapokosea fanya maamuzi ambayo hakuyategemea utaenda kuathiri mfumo wake wa ndani na kumpa adhabu ya muda mrefu. Kwa mfano mfanyakazi anapokosea na huku moyoni akiwa anajua kazi hamna tena lakini akakuta haujamfukuza huku moyoni mwako ukiwa umesamehe na hauna kinyongo, ukachukua sababu ya uzembe wake kama funzo na ukawa unaziandaa njia za kuziba mwanya wa uzembe huo bila kuongea chochote kwa huyo aliyesababisha uzembe ukamuacha aendelee na kazi kila siku akija asubuhi anategemea akute barua ya kumfukazi kazi kwa sekretari lakini anakuta sivyo. *Hakuna mfanyakazi atakaekuwa makini* kama huyo katika kufanya kazi.

Kwasababu hata ikimfukuza kazi haitafanya ile hasara ilipwe, Leo hii huyu aliyelisha mifugo yako ukaichukua na kuipeleka kwa mwenyewe na sio ofisi ya kijiji bila kuongea chochote, mwenye mifugo anaweza akakesha usiku akiwaza nini utakachoenda kukifanya akisikia mfugo unaguna tayari anahisi labda mifugo Itakufa hivyo hiyo hali itamsumbua sana tofauti na unavyofikiri. Na hauwezi kufa njaa utakachotakiwa kukifanya ni njia za kufanya uweze kupata mazao kwa njia nyingine kama yalikuwa ya chakula na hautakufa njaa nature itafanya kazi yake. Kwasababu hata ukilipwa faini mazao hayataota na wala haiwezi kuwa sawa na jasho ulilolimwaga.

Hahaha pagumu hapo lakini ndio ukweli wenyewe unakuwa tofauti kabisa na uhalisia. Lakini njia hii inafanya kazi kwa mtu mwenye akili timamu sasa sijui kama unaweza kuajiri mtu ambae hana utimamu kichwani.

Kwanini huyu unaemuona kama adui Kwasababu amekusababishia matokeo hasi utumie hii njia isiyoonekana ambayo inakutaka uendeleo na huyo unaemuona ndo adui wako kwasasa Kwasababu; ngoja upate msaada wa sheria hapa moja kati ya sheria za nguvu/uwezo sheria namba mbili **laws of power** inasema *“be wary of friends they will betray you more quickly, for they are easily aroused to eny. They also become spoiled and aroused to eny, they also become spoiled and tyrannical. But hire a former enemy and he*

will be more loyal than a friend because he has more to prove. In fact you have more to fear from friends than enemy. And if you have no enemies find a way to make them”.

Tukimalizia uhusika wa pili wa kihisia hapa ni pale mtu anakuchukia kutokana na mafanikio yako, yawe ni ya kikazi au yakielimu furahi kwasababu yeye ndiye chachu ya wewe kufanya vizuri na hata akikukosoa amini kuwa ni kweli kwa kuwa hatakuwa mnafiki. Hivyo huna budi kusamehe na kufurahia uwepo wake mwanafilosofia huyu anaitwa [Voltaire](#) anasema **“The best is the enemy of good”**. Jitahidi uweze kusoma na kuelewa huo ndo mwisho wa chapisho hili la kwanza.

“shukrani za pekee ziende kwa wale wote waliohusika kuandaa toleo hili kwa namna moja ama nyingine, Shukrani nyingi zimfikie Hizza Athuman pamoja na Jonathan Oscar kwa uhusika wao”

Author

MWL. HABER FARADAY

Mawasiliano ni

+255625934471

+255759311893.